# Nipashe

Jumatatu Machi 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581248

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


MID WEEK JACKPOT!

TZS. 508,027,160

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Jicho** kisiasa, kiuchumi ujio Makamu wa Rais wa Marekani

UKURASA 3

## Kinana aishauri BAKWATA ijenge shule za ufundi UK. 5

# Rushwa ya ngono bado shida sokoni

• **Udadisi** wabaini wajasiriamali wanaitoa ili kupata vizimba... *Endelea Ukurasa 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa mwakilishi wa TAHLISO, Amon Mugeta, alipotembelea mabanda ya maonyesho katika semina ya CRDB Bank Uwekezaji Day jijini Dar es Salaam jana. Wengine kutoka kushoto ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nauye, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela na Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Prof. Neema Mori. **Habari Uk.4 PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simulizi mhasibu wa benki alivyotekwa, kuchomwa moto UK.2


SPECIAL SUPPLEMENT ON COMPLETION OF TWO YEARS UNDER THE ABLE LEADERSHIP OF



HER EXCELLENCY DR. SAMIA SULUHU HASSAN

The Guardian Limited will publish a special supplement with **"The Guardian"** and **"Nipashe"** Newspapers, with a special report focusing on the achievements of the Government under the leadership of President **Dr. Samia Suluhu Hassan**

20th March 2023

We wish to invite you to be a part of this special supplement by publishing your **Special features, Congratulatory messages, Advertorials** and **Advertisements.**

The Guardian Nipashe

TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

617309101



MICHEZO MAYELE AANZA KUIGUSA SIMBA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikabidhi cheti kwa Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Diana Mwakitwange, kwa udhamini wa kampuni hiyo kwenye Mkutano Mkuu wa Tano wa Mwanamke Kiongozi 2023 ulioandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rushwa ya ngono bado shida sokoni

**Na Elizabeth Zaya**

UMOJA wa Wanawake wa Kutetea na Kupinga Ukatili wa Kijinsia (TAPO) Tabata jijini Dar es Salaam, umesema kundi la wanawake wanaojishughulisha na ujasiriamali sokoni, linakumbana na rushwa ya ngono.

Mkurugenzi wa TAPO Tabata, Stella Mbaga, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika mkutano uliowakutanisha wanawake zaidi ya 250 wanaofanya biashara sokoni kutoka Buguruni, Bonyokwa, Msimbazi na Tabata mkoani Dar es Salaam, ikiwa ni mwendelezo wa kuadhimisha Siku ya Wanamke Duaniani.

Ni kauli isiyopishana na taarifa iliyotolewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) takriban miaka mitatu iliyopita kwamba asilimia 28 ya kinamama wajasiriamali na wanafunzi wa vyuo mbalimbali nchini wanatumikishwa kwa aina hiyo ya rushwa.

Katika mkutano huo, Stella alisema: "Kinamama wengine hadi wananyimwa vizimba vya kuweka biashara zao sokoni, wanaambiwa mpaka watoe rushwa ya ngono. Hii ni hatari na tunatakiwa tuungane kupambana nayo. "Na hili tumelibaini wakati tukitoa elimu kwa wanawake namna mbalimbali ya kupambana na kukabiliana na ukatili. Wanawake wengi huko sokoni wanakumbana na aina hii ya rushwa."

Majasiriamali Sharifa Kharid alidai kukumbana na kushawishiwa kutenda jinai hiyo ya rushwa ya ngono na ikawa kikwazo kwake kufanya biashara alipokataa kuitoa kwa mwenye kizimba, japo hakutaja jina la soko alikokumbana na ukatili huo.

"Mimi huwa nauza pilipili za kusaga kwa kusambaza kwenye masoko mbalimbali. Ilifika mahali kwenye baadhi ya masoko niliacha kupeleka bidhaa zangu kwa sababu wale wanaume niliokuwa ninawapelekea walisema mpaka nitoe rushwa ya ngono ndipo niwe ninapeleka mzigo kwao.

"Na nina ushahidi wa rafiki yangu wa karibu alikwenda kuomba kizimba sokoni, Mwenyekiti wa Soko akamwambia mpaka atoe rushwa ya ngono. Alikubali kutoa na kibaya zaidi hata kizimba chenyewe hakupata," alidai.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Uwezeshaji Wanawake (Women Fund), Mary Lusimbi, alisema kuna haja ya wanawake kujitafakari zaidi namna ya kuongeza nguvu ya kupambana na vitendo hivyo vya ukatili ili kusaidia kizazi kijacho kuepukana na tatizo hilo.

"Bado wanawake wanahitaji kujitafakari na kuhakikisha wanapambana kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo rushwa ya ngono, ili kizazi kijacho kisikumbane na tatizo hilo, hususani katika mikakati tunayoitumia kupambana nalo.

"Tunapaswa tupambane zaidi na kujitafakari kuhusu suala hili ili kizazi kijacho kisilikute, kikute limekwisha. Tunataka hili jambo libaki kuwa historia, tunataka ifike wakati Siku ya Mwanamke tunacheza na kufurahia na sio tena kuendelea kulalamika kuhusu suala hili," alihimiza.

Pia alisema jitihada zinahitajika kuwakwamua wanawake kimtaji, hususani wenye kipato cha chini zaidi, akibainisha kuwa mfuko huo umeendelea kuwawezesha wanawake hao kiuchumi mijini na vijijini.

Mwanaharakati na Mwezeshaji wa Masuala ya Wanawake na Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Gema Akilimali alisema imefika wakati wanawake wasikubali kula njama kuficha watu wanaoshiriki vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Mnano Novemba 26, 2019, katika wasilisho lake kuhusu Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Intelijensia wa TAKUKURU, Emmanuel Kiyabo, alisema rushwa inayohusu ngono nchini ni kubwa kuliko ya fedha.

Katika maadhimisho hayo yaliyoandaliwa kwa ushirikiano wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Mtandao wa Wanawake (WFT), TAKURKU na Jeshi la Polisi, Kiyabo alisema asilimia 28 ya wanawake wanaofanya biashara ndogo na wanafunzi wa vyuo wanatumikishwa kwa rushwa ya ngono.

**UHUJUMU UCHUMI**

Rushwa ya ngono kwa sasa ni kosa linaloangukia kwenye jinai ya uhujumu uchumi na adhabu yake ni kifungo cha mpaka miaka 20 gerezani.

# ACT yataka maridhiano katika migogoro ya ardhi

**Na Julieth Mkireri,** TUNDURU

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kufanya maridhiano katika migogoro ya wakulima na wafugaji kama inavyofanya kwenye sekta zingine.

Pia kimeitaka serikali kutumia majukwaa rasmi kama Kamati za Ushauri za Wilaya na Mikoa kujadili masuala hayo kwa upana na kuhusisha wawakilishi wa wakulima na wafugaji ili kujenga maelewano miongoni mwao.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na wananchi wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.

Kwa mujibu wa Shaibu, majimbo yote waliyopita wamekutana na vilio vya wakulima kuhusu uhusiano wao na wafugaji, wakilalamika kuvamiwa na wafugaji kwenye mashamba yao na mifugo hiyo kula mazao yao.

"Migogoro hiyo imesababisha kuwa na mapigano baina ya wakulima na wafugaji, mapigano yanayohatarisha amani na usalama nchini, tatizo hili limekuwa kubwa zaidi kwenye Wilaya za Tunduru, Ruangwa, Nachingwea, Liwale, Lindi Vijijini na Kilwa," alisema.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema kuwa hata baada ya uchaguzi, chama hicho kimeendelea kuimarisha demokrasia na kuwatetea wananchi nje ya serikali na Bunge.

Alisema chama hicho kiliamua kuunda Baraza Kivuli nje ya Bunge na kuwa na wasemaji wa chama hicho ambao wataendelea kutatua kero za wananchi wakiwa nje ya serikali.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara, Dorothy Semu, alisema wananchi wengi wanakumbana na kikwazo cha kushindwa kulipa gharama za afya kutokana na hali zao duni kiuchumi.

# Simulizi mhasibu wa benki alivyotekwa, kuchomwa moto

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

BABA mzazi wa aliyedaiwa alikuwa mhasibu wa Benki ya Boa Tawi la Kahama, Neema Towo, amesema moto unaodaiwa kuwa ndio ulisababisha kifo chake ukiangaliwa vizuri huenda ukawa siyo kiini.

Amedai figo za mwanawe ziliharibika kutokana na kinachodaiwa kudungwa sindano ya sumu na walipoelezwa hali hiyo hospitalini, mmoja wa ndugu alikuwa tayari kujitolea lakini kabla ya hatua hiyo, binti yake alifariki dunia.

Akizungumza jana wakati wa ibada ya kuaga mwili wa marehemu huyo kwenye Kanisa la KKKT Tumbi, Kibaha mkoani Pwani kabla ya mwili huo kusafirishwa kwenda Kilimanjaro kwa ajili ya maziko, Ndeonasia Towo, alisisitiza watu wanatakiwa wapate taarifa sahihi kuhusu kifo cha mwanawe na si kuzungumzia mambo wasiyoyajua na kuyaweka kwenye mitandao.

Alisema watu wasidhani kuwa mwanawe alipoteza maisha kutokana na kujiingiza kwenye tamaa, pia mambo yasiyo na maadili, kwa kuwa watoto wake wote wawili amewatunza vizuri kwa kuwapa mahitaji muhimu ikiwamo elimu.

"Mwanangu hakuwa na rafiki wa kiume hapa Kibaha na alikuwa aolewe mwaka huu, na alikuwa shupavu, ndiyo maana baada ya tukio hilo alikimbia umbali mrefu na kufika kwenye nyumba walikomkuta anapiga kelele na nikapigiwa na kujulishwa tukio hilo," alisema.

Alishauri vyombo vya usalama viachwe vifanye kazi yake ili taarifa zitoke sahihi kwa kuwa baadhi ya watu wanatoa taarifa zisizo sahihi kuhusu mwanawe.

"Msirushe picha au kutoa taarifa kwani mnatoa habari msizojua, msitoe taarifa holela, acheni vyombo husika kwani simu zake zinafuatiliwa, utakamatwa, mimi sitoi taarifa, ninyi mnatoa taarifa mnazosikia hamzijui," alitahadharisha.

Towo alibainisha kuwa mwanawe hakutekwa kwa kutumia pikipiki, bali alitekwa kwa kutumia gari, akiwaonya mabinti na wanawake dhidi ya tabia za kupewa lifti au kudanganywa kirahisi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mharakani, Kibaha ambako familia hiyo ya marehemu inaishi, Eliamini Mgonja alidai kuwa watu waliohusika na tukio hilo watapatikana "kwa kuwa damu ya mtu siyo kitu cha mchezo".

Titus Saidaya mmoja wa wazee wa Kanisa la KKKT Tumbi, akitoa salamu za pole kwa familia hiyo kwa niaba ya kanisa, alisema binti huyo alikuwa muumini hai wa kanisa lao na siku ya kutekwa alikuwa kwenye ibada kanisani.

Mkuu wa Kanisa la KKKT Jimbo la Magharibi, Anta Muro, wakati wa mahubiri yake, aliwataka waumini wa kanisa hilo kutumika vyema katika shughuli za kanisa na za kijamii ili kuisaidia serikali kudumisha amani na upendo.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Jeshi la polisi Mkoa wa Pwani lilitoa taarifa ya binti huyo (30), mkazi wa Kwa Mbonde, Kibaha kufariki dunia baada ya mwili wake kumwagiwa mafuta yanayodhaniwa kuwa ni ya petroli kisha kuchomwa moto na watu wasiojulikana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani Pius Lutumo alisema tukio hilo lilitokea Machi 3 maeneo ya Mitamba.

HABARI KITAIFA

# Padri akemea kushamiri vitendo ushoga, ulawiti

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

PADRI Constatine Luhimbo, amesema ni vyema Wakristo wakajenga tabia ya kuelimishana maneno ya Mungu, ili kuwa na mioyo yenye hofu ya Mungu kwa kuwaepusha kutenda matendo maovu ya ndoa ya jinsia moja ambayo ni chukizo kwa Mungu.

Padri huyo wa Kanisa Katoliki Kigango cha Utatu Mtakatifu Parokia ya Kihonda Jimbo la Morogoro Mjini, alisema hayo jana kwenye ibada ya Jumapili ya tatu ya Kwaresma iliyofanyika kwenye kanisa hilo.

"Nilishuhudia kwenye mtandao wa kijamii mwanaume kutoka Kenya akiwa amevaa shela na tai yake, anaolewa na mzungu, huku akionekana mwenye furaha kabisa, tunaipeleka wapi dunia?" Alihoji.

Alisema jamii imemsahau Mungu na kuanza kujiingiza kwenye mambo ya ndoa za jinsia moja, yaani mke kwa mke au mume kwa mume jambo ambalo ni kinyume mbele za Mungu.

"Kama Mungu alituleta duniani ili tuje kuzaana, alisema nendeni mkaujaze ulimwenguni, sasa ndoa za jinsia moja kweli hapo kuna kuujaza ulimwengu, au kutafuta hasira ya Mungu, tumjue Mungu na kuyaacha maovu hasa wakati huu wa Kwaresma," alisema.

Alisema matendo hayo yalitendwa katika miji ya Sodoma na Gomola na kumchukiza Mungu ambaye aliwasha moto na wote wakateketea, lakini bado jamii haielewi na yeye haelewi kwa nini watu wanasahau tukio hilo kubwa.

Alisema inawezekana matokeo yanayojitokeza sasa ni sehemu ya kukosa hofu ya Mungu na kama kila mmoja akiwa mwalimu kwa mwenzie na kumfanya awe na hofu ya Mungu ndani yake itasaidia kupunguza au kuondoa nia za matendo maovu mioyoni mwao.

Alisema ifike mahali kila mmoja aweke imani, matumaini na upendo ndani yake hali itakayosaidia kumweka karibu na Mungu na kuacha kuwaza kufanya maovu.

# Jicho kisiasa, haki ujio Makamu Rais wa Marekani

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, anatarajia kufanya ziara nchi za Tanzania, Ghana na Zambia, kuanzia Machi 25 hadi Aprili 3, mwaka huu, huku wachambuzi wa siasa na haki za binadamu wakisema ni matokeo ya kuimarika kwa haki za binadamu na utawala bora.

Aidha, wamesema ni muhimu Tanzania ikajipanga kueleza changamoto zilizopo kwenye diplomasia ya uchumi pamoja na namna ya uendeshaji wa demokrasia bila kuharibu mila na desturi za nchi.

Kiongozi huyo anakuwa watatu wa ngazi ya juu ya taifa hilo kuitembelea Tanzania tangu rais wa awamu ya nne, wengine ni pamoja na Rais mstaafu Baraka Obama aliyefanya ziara ya kikazi Julai Mosi, 2013 na baada ya kustaafu alifika tena nchini kwa ziara ya mapumziko Julai 2018.

Mwingine ni Rais mstaafu George Bush, aliyefika nchini Februari 16, 2008 na kupata nafasi ya kuzindua mpango mpya wa kusambaza vyandarua maalum kwa ajili ya kuwalinda na malaria watoto wenye umri kati ya mwaka mmoja hadi mitano.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wachambuzi wa masuala ya kisiasa na diplomasia wanasema ziara ya kiongozi huyo inaonyesha kuridhishwa na mwenendo wa demokrasia nchini, hasa Rais Samia Suluhu Hassan alivyoweza kuliweka pamoja taifa.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema ziara zozote za viongozi wakubwa zinakuwa na manufaa ya kuboresha uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi hizo na kwamba Tanzania imekuwa kwenye nafasi nzuri.

"Viongozi hawa wakuu wanapopanga ziara zao kwa nchi zinazozungumza utawala bora na haki za binadamu huwa wanaangalia vitu vingi sana ndio watembelee.

Hii inaonyesha Tanzania ni ya kidemokrasia na inaheshimu haki za binadamu, ni ishara nzuri kwa namna mambo yanavyoendelea nchini kwamba tupo vizuri inaridhisha," alisema.

Pia alisema ziara hiyo itafungua fursa za kibiashara baina ya Watanzania na Marekani, ikiwamo kujadili vikwazo vilivyopo na namna ya kuviondoa.

Mchambuzi wa masuala ya siasa, Nassoro Kitunda alisema ni ziara muhimu kwasababu kwenye masuala ya kidiplomasia baina ya nchi hizo yamekuwapo kwa muda mrefu, ujio wake unaimarisha zaidi diplomasia iliyopo kwa sababu kuna biashara baina ya nchi hizo kupitia soko la AGOA, Tanzania inanufaika inapeleka bidhaa bila kodi wala changamoto.

Alisema bado kuna changamoto kwenye mifumo ya kibiashara, kuna korosho, kahawa na pamba lakini manufaa ni madogo hivyo ni muhimu.

"Inaweza kuwa sehemu muhimu juu ya kujua hasa hali halisi ya Tanzania kwa masuala ya kigeni, tangu uhuru tulikuwa na misimamo yetu ya kimtazamo mambo ya demokrasia na diplomasia, tuwape ujumbe juu ya demokrasia yetu, wakati mwingine hawafahamu kinachoendelea nchini, ni muhimu kuwaonyesha mipaka, kumktadha, tamaduni, mila na desturi zetu," alisema na kuongeza:

"Rais Samia aliwaeleza vijana kuheshimu mila na desturi wasiwe wepesi kupokea tu. Wanapokuja wakuu wa nchi wanakuja na ajenda zao na kwamba ni muhimu usiwe wa kusikiliza bali nchi kusema ya kwetu tunayoyaamini na kuyasimamia hasa diplomasia ya uchumi hasa inayoonekana ni ya upande mmoja hasa nchi zilizoendelea."

Mhadhiri na Mtaalamu wa Biashara na Uchumi wa Chuo cha Biashara (CBE), Mariam Tambwe, alisema ugeni huo utafungua mipaka ya nchi zote mbili kibiashara kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa mataifa yote kunufaika na fursa zilizopo kibiashara.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ikulu ya Marekani wiki iliyopita, Kamala atakuwa kiongozi wa 18 mkuu wa Marekani kuzuru Afrika, mwaka huu.

Inaelezwa kuwa ziara hiyo huenda ikawa inaandaa mazingira ya kuwasili kwa ahadi ya Rais wa Marekani, Joe Biden, kuja barani humo aliyoitoa kwenye Mkutano wa Viongozi wa Marekani wa Afrika huko Washington DC Desemba 2022.

Inabainishwa kuwa hadi sasa ziara za mke wa rais, Jill Biden nchini Namibia na Kenya zinachukuliwa kuwa za hadhi ya juu zaidi sambamba na ya Waziri wa Fedha wa Marekani, Janet Yellen ambaye alikuwa Senegal, Afrika Kusini na Zambia Februari, mwaka huu.

Mshauri mkuu wa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika Taasisi ya Amani ya Marekani, Edward Burrier, alisema ziara zilizopangwa za wajumbe wa Marekani barani Afrika sio za kawaida kwasababu wamekuwa wakienda zaidi ya ziara za kawaida za viongozi wa serikali.

"Tangu Januari, mwaka huu kwa kuhesabu tayari viongozi 17 akiwamo mke wa rais, wajumbe hao wamefika katika nchi 11 za Afrika," alisema.

Aliongeza kuwa Afrika Kusini inaangaziwa zaidi katika ratiba ya safari hiyo kwasababu ya umuhimu wake kama lango la kuingia Afrika kwa diplomasia ya Marekani.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 10/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SHABANI SWALEHE NCHIRA wa KISASA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA SWALEHE SHABANI NCHIRA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 14 Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo Tarehe 13 Mwezi 02 Mwaka 2023.**



**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala Iugala, Nala Segu kukamilisha malipo ya viwanja hivyo mapema.

Mwananchi au taasisi itakayoshindwa kulipia kiwanja hadi kufikia tarehe 25 Machi, 2023 atambue kuwa kiwanja hicho kitauzwa kwa mteja mwingine ili kuboresha huduma katika Halmashauri bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**

Joseph C. Mafuru
**MKURUGENZI WA JIJI**
**DODOMA**

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
S.L.P. 1249,
DODOMA

217303602

# Majaliwa ataka vijana, wanawake waichangamkie programu ya CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa rai kwa vijana na wanawake nchini kuchangamkia programu ya uwezeshaji kiuchumi iliyozinduliwa na Benki ya CRDB kwa kushirikiana na Tume ya TEHAMA (ICTC) na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kuboresha ubunifu wao za kibiashara.

Alitoa rai hiyo jana wakati wa semina ya Uwekezaji na Fedha ya Benki ya CRDB, iliyopewa jina la 'CRDB Bank Uwekezaji Day' iliyokwenda sambamba na uzinduzi wa taasisi ya hisani ya CRDB Bank Foundation pamoja na programu hiyo ya IMBEJU ambayo inalenga kutoa mafunzo, ushauri na mitaji wezeshi kwa vijana na wanawake.

Waziri Mkuu alisema programu hiyo imekuja kutoa suluhisho kamili kwa biashara changa za vijana na wanawake nchini kwa kuzijengea uwezo wa kujiendesha hususani kupitia mafunzo ya kimkakati ambayo yamepangwa kutolewa kwa kushirikiana na ICTC, COSTECH pamoja na wadau wengine katika programu za uwezeshaji wanawake kupitia vikundi.

"Ukweli ni kuwa tatizo la kushindwa kuendelea kwa biashara changa si kukosekana kwa mitaji. Mitaji ipo na taasisi zetu za fedha zipo tayari kufadhili, lakini hatari ya uchechefu ni kubwa kwani biashara changa nyingi zimekuwa zikishindwa kujisimamia. Niwashukuru Benki ya CRDB kwa kuliona hili na kuambatanisha programu ya IMBEJU na ushauri na mafunzo," alipongeza.

Waziri Mkuu aliwataka vijana na wanawake kutumia vizuri mitaji watakayopewa kwa kuwekeza katika maeneo waliyoyaainisha kupitia mipango yao ya biashara, huku akiwasisitiza kuwa waaminifu.

Pia alizitaka taasisi za serikali kutoa fursa kwa vijana waliokuja na ubunifu unazoweza kutatua changamoto za jamii, akitolea mfano wa vijana waliobuni mfumo wa kuongoza magari barabarani kupewa fursa na Wizara ya Ujenzi.

Waziri Mkuu aliipongeza Benki ya CRDB kwa kuja na programu hiyo na kusema inaendana na dira ya serikali ya kuchochea ubunifu kwa vijana na wanawake ili kutengeneza ajira na kuchochea maendeleo nchini.

Aliwahakikishia vijana kuwa serikali ipo pamoja nao katika kufanikisha ubunifu wao unakuwa na tija kwao na kwa jamii.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema programu ya IMBEJU itakwenda kuchochea uanzishwaji wa bidhaa na huduma mpya zinazoendana na mazingira na mahitaji halisi ya Watanzania. Nape aliwataka vijana kutumia fursa hiyo kuja na ubunifu utakaoshindana ndani na nje ya nchi.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohammed, aliwahimiza vijana na wanawake kutoka Zanzibar kuitumia fursa hiyo vizuri, huku akibainisha kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeendelea kuboresha mazingira ya kuchochea ubunifu na ukuaji wa biashara changa na kuhakikisha programu wezeshi kama IMBEJU zinatekelezwa kwa mafanikio.

Akifafanua sababu za kuanzishwa kwa programu ya IMBEJU, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Prof. Neema Mori, alisema programu hiyo ni sehemu ya jitihada za Benki ya CRDB katika kuchochea maendeleo na kujenga ujumuishi wa kiuchumi kwa vijana na wanawake.

Prof. Mori alisema IMBEJU ni sehemu ya programu endelevu ambazo zitakuwa zinatekelezwa kupitia kampuni tanzu ya CRDB Bank Foundation ambayo imepewa jukumu la kubuni, kuanzisha na kusimamia miradi endelevu ya uwezeshaji katika jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema programu ya IMBEJU ina malengo makubwa ya kuwezesha vijana na wanawake wengi kukuza biashara zao ili kujikwamua kiuchumi wao na familia zao huku wakitoa mchango kwa taifa kupitia kulipakodi za biashara, pia kutoa ajira kwa Watanzania wengine.

Nsekela alisema pamoja na mtaji wa Sh. bilioni tano ambazo zimetengwa, Benki ya CRDB kwa kushirikiana na Tume ya TEHAMA na COSTECH pia itakuwa ikitoa mafunzo ya uendeshaji wa biashara.

Alisema programu hiyo inalenga biashara za wanawake na biashara changa za vijana katika sekta mbalimbali huku msisitizo ukiwekwa katika ubunifu wa teknolojia.

Akieleza namna ya kushiriki katika programu ya IMBEJU, Mkurugenzi Mkuu wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa, alisema ili kupata mitaji wezeshi vijana na wanawake watahitajika kupitia mafunzo na baada ya kuhitimu wataunganishwa na akaunti ya IMBEJU kisha kupatiwa mitaji.

"Kwa upande wa biashara changa za vijana, maombi yatawasilishwa kupitia tovuti za Tume ya TEHAMA na COSTECH, kisha watapitishwa katika hatua mbalimbali za mafunzo. Wanawake wao watapitia katika matawi yetu, ambako watafanyiwa mafunzo kabla ya kupewa mitaji," alifafanua.

Akizungumza kwa niaba ya vijana wenye biashara changa, Mkurugenzi Mtendaji na Mwanzilishi wa Kampuni ya HACK IT, aliishukuru Benki ya CRDB kwa kuja na programu ya IMBEJU, huku akiwahamasisha vijana wengine kutumia fursa hiyo vizuri ili iwe na manufaa kwa vijana wengi zaidi.

Semina ya CRDB Bank Uwekezaji Day mwaka huu 2023 imehudhuriwa na washiriki zaidi ya 7,000 ambapo sehemu kubwa ni vijana ambao walishiriki kupitia mtandao toka pande zote za nchi, Bara na Visiwani. Semina hiyo ilihusisha mijadala mbalimbali ya jinsi ya kuongeza uwezeshaji kwa vijana na wanawake na kukuza ubunifu wa kiteknolojia.

**UBALOZI WA DENMARK, NORWAY, BRITISH HIGH COMMISSION NA EUROPEAN UNION**
**DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Denmark, Norway, British High Commission na European Union watauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani, Magari na Pikipiki tarehe18 March, 2023 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza Fenicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa set, Zanzibar beds, Chest drawer, Dining table, Chairs, Book case, Office desk, File cabinet, Shelves, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, Upright Freezer kubwa, Washer, Dryer, A/c split units, Photocopy m/c, TV set, Computer set, Printers, 4 Sets Professional Music Systems, Safe, Solar water heater, Lawnmower, Generator 3KVA Na vingine vingi.

**Magari/Pikipiki yataanza kuuzwa saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser GX Station Wagon | 1HZ Diesel Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado | 2TR Petrol Engine | 2010 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Murano Station Wagon | Z250 Petrol Engine | 2006 | Umelipwa |
| 1 | Ford Escosport Station Wagon | FY5 Petrol Engine | 2015 | Haujalipwa |
| 2 | Honda Motorcycle | XR 125L & CT200 Petrol | 2012 | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 15 mpaka 17 March, 2023, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 24 March 2023 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**Cell Number- +255 0754 284 926** **Dar es salaam**
**E-mail: universalauction@hotmail.com** **Insta:universalauctioncentre**

# Mradi wa Bil. 140/- kutatua kero ya uhaba wa maji Ruvuma

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

SERIKALI imetia saini mkataba wa Sh. bilioni 145.7 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji wa miji 28 kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Mkataba huo ulitiwa saini juzi kati ya serikali na Mkandarasi, Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation mkoani Ruvuma.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema ujenzi wa mradi huo unatekelezwa kwa miezi 12 kuanzia juzi.

"Kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa maji wa miji 28 kwenye Manispaa ya Songea kutaleta manufaa makubwa ikiwamo SOUWASA (Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea) kuongeza uwezo wa kuzalisha maji kutoka lita milioni 11.58 kwa siku hadi kufikia lita milioni 42.581 kwa siku," alisema.

Aliongeza kuwa mradi huo wa maji unakwenda kumaliza kero ya maji kwenye Manispaa ya Songea kwa kuwa upatikanaji wake utakuwa wa uhakika, mradi huo ukitarajiwa kutoa huduma kwa wananchi 440,794.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Nadhifa Kemikimba alisema mradi huo utakapokamilika, utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi wa Songea hadi mwaka 2045.

"Mradi huu utahusisha ujenzi wa bwawa lenye uwezo wa kujaza maji lita milioni 4.8, ujenzi wa mtambo wa kuchuja maji lita milioni 16 kwa siku, ujenzi wa matangi ya maji lita milioni tisa.

"Pia kulaza mabomba yenye urefu wa kilometa 10.5 yatakayosafirisha maji kutoka kwenye mabwawa hadi kwenye matangi," alisema.

## Public Notice

Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) a non-governmental organization with a certificate of compliance under the Non-Government Organizations Act of 2002 based in Dar es Salaam Tanzania wishes to inform the general public that it has signed a grant agreement with the ABA for the year 2023-2024 to implement a project in ten (10) villages of five (5) administrative wards of Tarime district in Mara region: Kemambo, Nyarero, Nyamwanga, Matongo and Gorong'a.

**The Name of the Project: ENHANCING PROTECTION OF ENVIRONMENTAL DEFENDERS IN AFRICA/.**

**Location: Tarime district, Mara Region**

**Amount: 28,214 USD**

**Donor: AMERICAN BAR ASSOCIATION (ABA)**

**Time frame: 2023-2024**

For further information please email: info@leat.or.tz

# Kinana aishauri BAKWATA iongeze nguvu ujenzi wa shule za ufundi

**Na Mwandishi Wetu,** LUSHOTO

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, amelishauri Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kufikiria kujenga shule za ufundi zitakazowawezesha vijana kupata ujuzi wa kujiajiri na kuwaingizia kipato.

Kinana alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati wa ufunguzi wa Msikiti Mkuu wa BAKWATA Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, alipokuwa mgeni rasmi wa hafla hiyo.

Ushauri huo wa Kinana unatokana na maelezo aliyopewa kuhusu majengo yatakayojengwa kwenye eneo hilo, yanayojumuisha shule ya msingi na sekondari.

"Mna mpango wa kujenga shule ya sekondari, shule za msingi. Kwa ushauri wangu jengeni shule za ufundi, shule za sekondari ni nyingi, shule za serikali ni nyingi, mkijenga shule mtataka watu walipie wakati serikali inatoa elimu bure.

"Tunao mfano wa shule za Jumuiya ya Wazazi zinapata tabu kwa sababu wanaokwenda kusoma wanatakiwa kulipa, lakini mwanafunzi akijua kuna shule ya ufundi inayofundisha uashi, ufundi umeme, udereva, ufundi magari, yuko tayari kulipa kwa sababu anajua atapata kazi.

"Shule ambazo tunasoma, nyingi zaidi ya cheti hakuna tunachopata, ni bora ukawa na cheti cha ufundi kuliko kumaliza kidato cha sita. Ukiwa fundi hata usipoajiriwa unaweza kujiajiri na mtu ukapata riziki yako ya kila siku," alisema Kinana.

Aliongeza: "Shule tunazofikiria kujenga iwe ya msingi au sekondari zilenge kufundisha vijana taaluma za mikono. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumesaidia kutengeneza ajira, ukimaliza ufundi ukienda kwa mtu atakwambia twende ukanijengee lakini ukimaliza chuo ukamwambia nimesoma siasa, atakwambia hakuna ajira."

Mbali na hilo, Kinana aliwasisitiza waumini wa dini ya Kiislamu kuongeza juhudi ya kusoma elimu dunia na elimu ya ahera.

Makamu Mwenyekiti Kinana alisema ana hakika waumini wengi wa dini hiyo wamejitahidi katika elimu ahera, lakini elimu dunia nayo waisome.

"Tusome na kufaulu vizuri ili tupate kazi na kazi sio serikalini tU, bali hata kwenye taasisi za kimataifa," alihimiza.

Pia alizungumzia tabia njema, akisema inatokana na mafunzo ya dini na kwamba hata Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza kuhusu kujenga taifa lenya maadili, umoja na watu wenye kuheshimiana.

**KAULI YA MUFTI**

Awali Mufti wa Tanzania Dk. Aboubakar Zuberi bin Ali alitumia nafasi hiyo kuhamasisha Waislamu kushiriki kikamilifu katika kuchangia ujenzi wa msikiti huo huku akielezea madhara ya fitna katika jamii ya Waislamu.

"Kwenye Uislamu kuna fitina, watu hawafikirii sana na Mungu ameitaja fitina mara mbili, Mwenyezi Mungu anaeleza ukubwa wa fitina inavyoharibu mambo.

"Akiwekwa imam baada ya siku mbili hafai, Waislamu tukiendelea na fitina hatutaendelea, hivyo ngazi ya wilaya, mkoa na taifa tuache fitna.

"Nimefanya utafiti na kubaini fitna imetuharibia, ukijenga msikiti mzuri wanakuja wanasema imamu wa zamani hafai, tuache kuchonganisha, unachukua fitna yako unakwenda kuchonganisha watu.

# 'Acheni kuwatelekeza wake wanaojifungua watoto wenye ulemavu'

**Na Shufaa Lyimo**

OFISA Tarafa wa Kibamba, Wilaya ya Ubungo mkoani Dar es Salaam amewataka wanaume kuacha tabia ya kutelekeza wake zao pindi wanapojifungua watoto wenye ulemavu, wakiwamo wenye mgongo wazi na vichwa vikubwa.

Beatrice Mbawala alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipotembelea Kituo cha Watoto Wenye Ulemavu (ASBAHT) kilichoko Kimara Temboni wilayani Ubungo na kuzindua nyumba ya matumaini kwa ajili ya wazazi wasio na ndugu wanaotoka mkoani.

"Ninaomba wanaume waache tabia za kutelekeza wake zao wanapojifungua watoto wenye ulemavu wa vichwa vikubwa na mgongo wazi, inapaswa watambue kuzaa mtoto wa aina hii ni mpango ya Mungu," alisema.

Beatrice aliwataka wanawake wasikate tamaa wanapozaa watoto kama hao na badala yake wapambane ikiwa ni pamoja na kuhudhuria kliniki ili wapate huduma mapema kabla tatizo halijawa kubwa.

Pia aliwataka wazazi wenye watoto wa aina hiyo wawapeleke hospitalini badala ya kuwaficha ndani.

Mlezi wa vijana wa chama cha wazazi wenye watoto waliozaliwa na ulemavu wa vichwa vikubwa na mgongo wazi, Norbert Kyando, alisema nyumba hiyo imekuwa ikisaidia wazazi zaidi ya 100 ambao hawana ndugu wanaotoka mikoa mbalimbali.

Alisema wazazi hao ni wale ambao walitelekezwa na waume zao kutokana na kuzaa watoto wenye ulemavu.

Alisema wamefanikiwa kuanzisha miradi mbalimbali ikiwamo ufugaji wa kuku wa mayai na kilimo cha bustani za mboga, kikiwapa manufaa ikiwamo kuhudumia kituo kwa chakula.

Santos Chuwa aliyezaliwa na tatizo la mgongo wazi na kichwa kikubwa, alisema kuwa mama yake alimsimulia namna baba yake alivyowatelekeza hospitalini alipozaliwa na matatizo hayo.

"Mama yangu alitelekezwa na baba aliponiona nimezaliwa na ulemavu, ilifika hatua akamwambia mama yangu anitupe. Ninamshukuru mama yangu alihangaika na mimi mpaka leo nimekua, ninafanya kazi, nina mke pamoja na mtoto mmoja," alisema Chuwa.

Mratibu wa chama hicho, Suma Mwaipopo, aliwataka wanawake wanaozaa watoto kama hao wasiwatupe, waendelee kuwalea kwa kuwa wanahitaji matunzo kama wengine.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## TAHADHARI KWA UMMA KUHUSU MATANGAZO YA KUGHUSHI YA AJIRA NA ZABUNI

**NAFASI ZA AJIRA**

Mchakato wa ajira wa Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP Ltd) na Wakandarasi wake kwa wafanyakazi wenye ujuzi na wasio na ujuzi upo wazi na bayana. Kampuni ya EACOP Ltd pamoja na makampuni ya Wakandarasi wanaohusika katika ujenzi wa Mradi wa EACOP hawaajiri wafanyakazi kwa njia isiyo rasmi au kwa kuhitaji malipo.

**MCHAKATO WA AJIRA WA EACOP NI BURE**

Hakuna mchakato wa ajira uliohalali wa Kampuni ya EACOP Ltd au Mkandarasi wake utakaohitaji malipo kwa ajili ya kuajiriwa katika nafasi zilizopo au zitakazo tangazwa hapo baadae.

**ZIFAHAMU KANUNI HIZI ZA AJIRA ZA KAMPUNI YA EACOP LTD PAMOJA NA WAKANDARASI WAKE:**

- Nafasi za ajira kwa wafanyakazi wenye ujuzi zinatangazwa angalau katika magazeti yanayosomwa sana ya kitaifa na kikanda, aidha nafasi hizo za ajira zinaweza kupatikana kwenye tovuti ya www.eacop.co.tz na tovuti za Wakandarasi wenyewe upande wa Ajira na Zabuni.
- Matangazo ya kazi kwa wafanyakazi wasio na ujuzi hubandikwa hadharani katika vijiji ambavyo shughuli za ujenzi hufanyika, kipaumbele daima hutolewa kwa waombaji ambao ni wakazi wa muda mrefu wa jamii zilizopo karibu na eneo la ujenzi.
- Wakandarasi wa Ujenzi na wawakilishi wa EACOP huwasiliana mara kwa mara kuhusiana na masuala ya ajira na dhamira ya kuwa na mchakato wa ajira ulio wa haki na uwazi.
- Mchakato wa ajira wa Kampuni ya EACOP Ltd na Wakandarasi wake daima huzingatia sheria za kazi za kitaifa na Viwango vya Kimataifa vya Ajira na Kazi.

**VIASHIRIA VYA MATANGAZO YA KUGUSHI**

- Ajira zilizotangazwa hazipo kwenye tovuti ya EACOP au ya Mkandarasi.
- Ada/malipo huombwa

**HUDUMA NA FURSA ZA UGAVI**

Kampuni ya EACOP Ltd. pamoja na Makampuni ya Wakandarasi hayaombi malipo kwa ajili ya mipango ya huduma ya siku zijazo, mipango ya haraka au Kupewa kipaumbele.

Kila mara maombi ya kuonesha nia (EOI) kwa ajili ya nafasi za ugavi yanapotangazwa, EACOP husambaza EOI katika jamii ya wafanyabiashara kwa ngazi ya taifa, mkoa na wilaya.

Endapo utaona matangazo yoyote ya kazi au tenda ya kughushi au yenye kutia mashaka iliyo ndani ya muda, tafadhali toa ripoti haraka kwenye ofisi za EACOP au wakandarasi zilizo karibu nawe, kituo chochote cha polisi au mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya ufafanuzi au ili kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

**ENDAPO UNAMASHAKA JUU YA UHALALI WA NAFASI ZA AJIRA, HUDUMA NA ZABUNI:**

- **Wapigie EACOP kwa simu ya bila malipo 0800 780 068**
- **Wasiliana na wawakilishi wa EACOP waliopo katika jamii.**

**KWA MAELEZO ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**

**EACOP Tanzania / Kwa Simu ya bila malipo: 0800 780 068 / Barua pepe:** info.tz@eacop.com

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga na mechi za kuamua hatima CAF

**JUMAMOSI** na Jumapili miamba ya soka nchini, Simba na Yanga, kwa mara nyingine tena itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye mechi ngumu zinazoweza kuamua hatima yao ya kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Wawakilishi hao wa nchi, kila mmoja anashika nafasi ya pili kwenye kundi lake, Simba ikiwa na pointi sita katika Kundi C la Ligi ya Mabingwa Afrika linaloongozwa na Raja Casablanca ya Morocco ambayo tayari imeshafuzu kutokana na kufikisha alama 12 ambazo zinaweza kufikiwa na 'Wekundu wa Msimbazi' hao pekee.

Hii ni kutokana na Horoya ya Guinea kuwa na alama nne huku Vipers ya Uganda ikiburuza mkia bila pointi wakati huu ambao kila timu imebakiza mechi mbili katika kundi hilo.

Kwa upande wa Yanga, nayo inashika nafasi ya pili na pointi saba kwenye Kundi lake la D katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, ikiwa nyuma ya US Monastir ya Tunisia ambayo ina alama 10 zinazoweza kufikiwa ama kupitwa na wawakilishi hao wa Tanzania pekee.

Hiyo ni kutokana na TP Mazembe ya DR Congo kuwa na alama tatu wakati Real Bamako ya Mali ikiwa na pointi mbili, wakati huu kila timu pia katika kundi hilo ikibakiza mechi mbili kabla ya kuhitimisha hatua hiyo ya makundi.

Kwa mantiki hiyo, wawakilishi hao wa nchi, Simba na Yanga, wanachotakiwa ni kushinda tu mechi zijazo ambazo zitachezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, ili kufuzu hatua ya robo fainali, vinginevyo zitajiweka katika wakati mgumu wa kusubiri matokeo ya mechi za mwisho.

Endapo Simba itapoteza mechi ijayo dhidi ya Horoya AC, italazimika kushinda mchezo wa mwisho ugenini dhidi ya Raja Casablanca na wakati huo huo ikiombea miamba hiyo ya Guinea kupoteza dhidi ya Vipers nyumbani jambo ambalo ni gumu.

Kadhalika, kwa upande wa Yanga, endapo watapoteza mechi ijayo nyumbani dhidi ya US Monastir, na wakati huo TP Mazembe wakishinda au kupoteza dhidi ya Real Bamako ugenini, hii ina maana mechi za mwisho ndizo zitakazoamua timu itakayoungana na US Monastir kutinga robo fainali.

Hivyo, ili kuondoa presha na kumaliza kazi hiyo mapema, Simba na Yanga iwe mvua ama jua, kinachotakiwa kwao ni ushindi tu Jumamosi na Jumapili, jambo ambalo Tanzania kwa mara ya kwanza itaandika rekodi ya kuingiza timu mbili hatua ya robo fainali kwa pamoja katika msimu mmoja wa michuano hiyo inayoandaliwa na kuratibiwa na Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Tunaamini hakuna njia ya mkato katika kulifanikisha hilo zaidi ya mabenchi ya ufundi ya timu hizo kufanya marekebisho madogo madago katika vikosi vyao ili kuweza kupata matokeo chanya kwenye mechi zao hizo.

Ingawa muda uliobaki wa siku nne hadi tano unaonekana kuwa mchache kwao, lakini sisi tunaona inawezekana kufanya marekebisho katika vikosi vyao na kupata ushindi hasa tukizingatia kuwa wawakilishi wetu hao wanakwenda kucheza na timu ambazo tayari wanazifahamu ubora na udhaifu wao, jambo ambalo pia hata wapinzani wao hao wanawafahamu.

Lakini matumaini yetu makubwa yanaongezeka zaidi kwa kutambua kuwa Simba na Yanga zitakuwa na faida ya mchezaji wa 12 uwanjani, ambaye ni mashabiki tunaoamini watajitokeza kwa wingi kuujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa ili kuzipa sapoti timu zao.

Hivyo, wakati huu wachezaji, mabenchi ya ufundi na viongozi wakiendelea na maandalizi ya ndani na nje ya uwanja kuelekea mechi hizo mbili, ni wakati sasa kwa kila shabiki na wadau wote wa soka kuanza kukata tiketi kwa wingi zaidi ili kwenda kuujaza uwanja siku hizo mbili na si kuujaza tu, bali kuzishangilia mwanzo mwisho ili kupata ushindi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Kipigo cha Al Ahly kiwe somo kwa mashabiki wa Tanzania

**SIPATI** picha kama Simba ndiyo ingefungwa mabao 5-2 dhidi ya Mamelodi Sundowns juzi kwenye Uwanja wa Loftus Versfeld, mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na si Al Ahly ya Misri.

Labda utashangaa kwa nini sijasema Yanga. Nasema Simba kwa kutokana na historia iliyojiwekea huko nyuma ya kutinga hatua ya robo fainali za Ligi ya Mabingwa na mara moja Kombe la Shirikisho, wengi wanasema haichezi vizuri kama ilivyokuwa wakati ule.

Simba inahukumiwa na historia, rekodi na kiwango chake yenyewe. Kipindi hicho ikiwa kwenye kiwango cha hali ya juu, huku ikiwa na kina Meddie Kagere, Chriss Mugalu, Rally Bwalya, Emmanuel Okwi, Nicolaus Gyan, James Kotei, Gerson Fraga, Thadeo Lwanga, na wengine wengi ambao waliifanyia makubwa, hivyo hadi leo hii mashabiki wa timu hiyo, na hata wachambuzi wanaitaka iwe kwenye hali hiyo hiyo. Na wengine wanadhani ipo kwenye kiwango hicho, ila kuna matatizo ya kiufundi ndiyo yanasababisha.

Ndiyo maana hadi leo wapo baadhi ya mashabiki na wachambuzi wa soka wanadhani tatizo la timu hiyo ni Kocha Mkuu, Robertinhp Oliveira, ambaye amezipa mafanikio makubwa Klabu ya Rayon Sport ya Rwanda na Vipers ya Uganda ambayo mpaka leo wanahaha na kocha, huku waliomchukua baada ya Robetinho wakimtimua kutokana na kufungwa na Simba kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa.

Simba ile iliyofanya makubwa, pamoja na kwamba baadhi ya wachezaji wameondoka, lakini ina wengine wengi ambao walikuwapo na bado wapo kwenye kikosi hicho kama Aishi Manula, Shomari Kapombe, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Joash Onyango, Erasto Nyoni, nahodha John Bocco na wengineo.

Ukiangalia kinachoipata Simba, ndiyo hicho hicho ambacho kinazipata timu nyingi kubwa za Afrika kama Al Ahly, TP Mazembe, na hata Mabingwa Watetezi, Wydad Casablanca, hawapo vizuri sana kama walivyokuwa msimu uliopita.

Hiki kinaitwa kipindi cha mpito, ambacho huzipata timu ambazo zimeshafanya makubwa kiasi, sasa zinaanza kuteremka taratibu.

Waswahili wana msemo wao mmoja kuwa anayekwenda juu kileleni ni lazima arejee chini. Hakuna anayeweza kukaa juu milele. Na pia kupata umaarufu si kazi kubwa, lakini kazi ni kuulinda. Wala isingewezekana kwa wachezaji hawa wa Simba kuendelea kuwa na kiwango kile kile walichokuwa nacho misimu mitano iliyopita, badala yake watakuwa wanateremka chini taratibu.

Sasa kuna watu walikuwa wanataka kuona ikicheza kama vile ilivyokuwa wakati huo. Ukiangalia wachezaji wengi wamechoka kwa sababu mbalimbali, hivyo kilichobaki wanacheza 'kikubwa' kwa ajili ya kupata ushindi na si kufurahisha watu jukwaani, mashabiki au wachambuzi.

Hicho pia kinaikumba Al Ahly, nayo ina kikosi ambacho kinahitajika kifanyiwe marekebisho makubwa msimu ujao, kwani msimu huu hakijaanza vema kabisa michuano hii na huenda kikakosa kuingia hatua ya robo fainali kwa mara ya kwanza baada ya msimu mingi kupita.

Kwenye Kundi B, Al Ahly ina pointi nne tu, ikiwa imeshinda mechi moja, sare moja na kupoteza mechi mbili dhidi ya Mamelodi Sundowns na Al Hilal ya Sudan.

Mamelodi ina pointi 10 na Al Hilal tisa, hivyo kama timu hizo zitapata ushindi kwenye mechi zinazofuata, basi Wamisri hao hawatavuka hatua hiyo.

Hali hiyo inazikuta timu nyingi baada ya kufanya vizuri kwa muda mrefu kwa sababu nyingi, ikiwamo wachezaji wake kushuka viwango, kutumika kwa muda mrefu bila ya kuwa na mbadala, kuridhika na mafanikio na mengine yanayofanana na hayo.

Al Ahly, Simba na hata Zamalek ni wakubwa waliolala, inawezekana zikawa hazipo kwenye wakati mzuri msimu huu, lakini hiyo ni kengele kwa viongozi wa timu hizo kuwa wanahitaji usajili mkubwa na wenye tija msimu ujao ili zirudi kwenye ubora wao uliozoeleka.

Robetinho kama ataachwa na kupatiwa wachezaji wa maana msimu ujao, Simba inaweza kuwa ya kutisha, kwani nadhani hata viongozi wenyewe watakuwa wamejifunza kutokana na makosa ya kutoyatumia madirisha mawili vizuri kwa kusajili wachezaji watakaoingia moja kwa moja kwenye kikosi, au kutoa changamoto kwa waliopo.

Mfano, hadi leo hii, hakuna changamoto yoyote kwa Kapombe na Tshabalala, na kama ni usajili inatakiwa wasajiliwa wachezaji wanaokwenda moja kwa moja kuchukua nafasi hizo na wao kuanza kupumzisha miili yao.

# Majaliwa aipongeza GGML kwa kuwainua wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameipongeza Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kuwawezesha wanawake walioajiriwa ndani ya kampuni hiyo kujiendeleza kielimu na kuwapa promosheni za nafasi mbalimbali ikiwamo uongozi pindi wanapohitimu mafunzo au masomo yao.

Pia ametoa wito kwa kampuni nyingine kutoa ufadhili wa mafunzo mbalimbali kwa wafanyakazi wanawake ili kuongeza tija katika matumizi ya kidijitali kama ilivyofanya GGML.

Majaliwa alitoa pongezi hizo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa Mahafali ya Nane ya Programu ya Mwanamke Kiongozi (FFT) iliyoratibiwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) ambapo jumla ya wahitimu 65 walitunukiwa vyeti wakiwamo wahitimu wanne kutoka GGML. Mmoja wa wahitimu hao, Tatu Tibashengwa ambaye alikuwa Msimamizi wa Udhibiti wa Ndani, amepandishwa cheo na kuwa Meneja Utawala Bora. Wengine waliohitimu kutoka GGML ni Changwa Mjella, Hellen Mallya na Flora Muhochi.

Akizungumzia hatua hiyo, Majaliwa alisema: "Nimefurahi kusikia wanawake kadhaa waliohitimu katika programu hii wamefanikiwa kupata nafasi za juu za uongozi kama dada yetu wa GGML (Tatu Tibashengwa), hayo ndio mafanikio tunayoyataka."

Alitoa wito kwa wanawake kujitokeza kwa wingi kushiriki katika programu hiyo kwa kuwa imeendelea kuwa na matokeo chanya kwa washiriki na kuleta mabadiliko makubwa kwenye utendaji wao wa kazi na kugusa maisha yao binafsi.

Pia aliwataka wanawake wote na Watanzania kwa ujumla kuendelea kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotokana na matumizi ya teknolojia katika kujenga uchumi wa kidijitali.

Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzanne Doran alisema kuwa tangu waanze programu hiyo kwa kushirikiana na ESAMI, wameshatoa mafunzo kwa wanawake 274 kutoka kampuni 79 wakiwamo wabunge na wawakilishi 150.

Awali akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya GGML, Terry Strong, Kaimu Meneja Rasilimali Watu, Dominic Marandu, alisema tangu mafunzo hayo yalipoanzishwa mwaka 2016, GGML imepeleka jumla ya wafanyakazi wa kike 17 katika programu ya kuwapatia mafunzo hayo ya FFT.

Alisema baadhi ya wahitimu wameteuliwa kwenye nafasi mbalimbali za uongozi ndani na nje ya kampuni hiyo, akiwamo Mjumbe wa Bodi ya STAMICO, Janeth Luponelo.

"Hivi sasa tupo katika mchakato wa kupendekeza majina ya wafanyakazi wengine wanne wa kike katika programu inayofuatia," alisema. Aliongeza kuwa GGML itaendelea kuongeza ujumuishwaji, usawa na kukubaliana na tofauti mbalimbali zilizopo kwenye makundi ya kijamii.

Akizungumzia promosheni aliyoipata kutoka GGML, mbali na kueleza kuipokea kwa furaha, Tatu aliishukuru kampuni hiyo kwa kutambua utendaji wake uliotukuka, ufanisi, ujasiri na kudumisha dhana ya usawa wa kijinsia mahala pa kazi.

"Ni sehemu ambayo wanawake wengine watavutiwa kufanya kazi na hata wenzangu walioajiriwa ndani ya kampuni, watapata hamasa ya kwamba inawezekana," alisema.

Aliahidi kuitumia nafasi hiyo kuwawakilisha wanawake vizuri, pia kuwapa miongozo wanawake wanaotaka kuwa viongozi kama yeye.




Meneja wa Tawi la Arusha Mjini wa Benki ya Azania, Bhoke Makore (wa pili kulia), akimkabidhi zawadi Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela (wa tatu kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo katika Kongamano la Wanawake na Vijana Wafanyabiashara Afrika lilioandaliwa na Mtandao wa Uwezeshaji Wanawake Tanzania (TAWEN) jijini humo wiki hii. Benki ya Azania ilidhamini mkutano huo. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa TAWEN, Florence Masunga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TGNP yataka mchakato wa Katiba uanzie kwenye rasimu

**Na Restuta James**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Gema Akilimali, amesema kuwa wanaharakati wanategemea mchakato wa Katiba mpya utaanzia kwenye Rasimu ya Pili ya Tume ya Katiba iliyoongozwa na Jaji mstaafu Joseph Warioba.

Akilimali alitoa maoni hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam alipozungumza na Nipashe kuhusu azma ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kufufua mchakato wa Katiba.

Akiwa mkoani Kilimanjaro Machi 8, mwaka huu, kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake iliyoandaliwa na Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), Rais Samia, aliahidi kwamba hivi karibuni atatangaza timu ya kushughulikia mchakato wa Katiba.

Akilimali alisema Tume ya Jaji Warioba, iliandika rasimu nzuri ambayo ilitokana na maoni ya wananchi na kwamba kufufuliwa kwa mchakato huo kuanzie kwenye rasimu hiyo.

"Tume ya Warioba ilipita kwa wananchi, ikaandika rasimu ya Katiba ambayo ilikuwa nzuri na sisi katika mitandao yetu tumeshasema kwamba haina hata kazi (timu ya kuandaa katiba); na watendaji wa serikali wapo ambao wanaweza kuendeleza tu ule mchakato," alibainisha.

Alisema hakuna sababu kwa serikali kutumia fedha nyingine kuanza mchakato huo, ambao alidai umeshagharimu fedha nyingi za umma na kutimiza kazi iliyotakiwa.

"Rasimu ile ni maoni ya wananchi, watendaji wa serikali wanachoweza kufanya ni kuangalia tu vipengele vidogo vidogo na kurekebisha lugha na kisha kuchapisha rasimu itakayopigiwa kura," alisema Akilimali.

Aliongeza kuwa: "Ile ndiyo ya wananchi, fedha ilitumika kubwa kwa hiyo hatuoni sababu ya kuanza na kitu kipya, hatuoni sababu ya kutumia rasilimali ya taifa kwa kazi ambayo ilishakamilika."

Naye bingwa wa Hisabati, Profesa Veridiana Masanja, alisema mchakato wa Katiba ulikwamishwa na wanasiasa na kutahadharisha kwamba mazungumzo na maridhiano ndiyo yatakayofanikisha upatikanaji wake.

Alitahadharisha kwamba ikiwa mchakato huo utaanza upya, serikali inapaswa kuangalia gharama ambazo zimekwishatumika, kilichopatikana na kinachotafutwa.

Mchakato wa kuandika Katiba mpya ulianza rasmi mwaka 2011 kwa kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 83/2011 ambayo iliunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoongozwa na Jaji Warioba.

Tume ya Jaji Warioba, iliratibu mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi na kuandaa rasimu ya kwanza ya Katiba ambayo kupitia uhariri wa Mabaraza ya Katiba ikapatikana Rasimu ya Pili ya Katiba. Mwaka 2013 ilitungwa Sheria nyingine ya Kura ya Maoni Na. 11/2013 ambayo iliunda Bunge Maalum la Katiba ambalo lilipokea rasimu ya pili ya Katiba.

Hata hivyo, mchakato ulikwamia kwenye Bunge hilo baada ya wajumbe kuvutana kiasi cha wanasiasa wa upinzani kususia wajibu huo.

Aidha, wajumbe wa Bunge ambalo waliendelea na mchakato huo waliandika Katiba inayopendekezwa ambayo makundi mengi waliipinga kutokana na kwamba ilibadilisha maoni ya wananchi yaliyokuwa yamewasilishwa kupitia Rasimu ya Pili ya Tume ya Jaji Warioba.

Mchakato huo ulikwama rasmi mwaka 2014 baada ya wanasiasa wa upinzani chini ya mwavuli wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) na wale wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kushindwa kufikia maridhiano huku wanaharakati na wadau mbalimbali wakitaka Rasimu ya Warioba ndio ipendekezwe kuwa katiba.

Baadhi ya mambo yaliyokwamisha mchakato huo ni kukosekana muafaka kwenye masuala ya Muungano, Tume Huru ya Uchaguzi, Mamlaka makubwa ya Rais, madaraka ya umma, haki za binadamu na utawala bora, mgombea binafsi na mgawanyo wa madaraka ya mihimili (Serikali, Bunge na Mahakama).

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUISHA TAARIFA ZA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) NA NAMBA YA UTAMBULISHO WA TAIFA (NIN)

***Dar es salaam, 10 Machi, 2023***

Kwa mujibu wa mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2022, Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Sura 438) kinampa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kumsajili na kumpa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) kila Mtanzania mwenye umri wa miaka kumi na nane (18) na kuendelea ambaye amesajiliwa na kuwa na Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN) inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Sambamba na hilo, mabadiliko hayo ya Sheria yanamtaka kila mwenye TIN kuhuisha taarifa zake ili ziwiane na taarifa za NIN. Utekelezaji wa Sheria hii ulianza rasmi tarehe mosi Januari 2023.

Katika utekelezaji wa Sheria hiyo, TRA inapenda kuumbusha Umma kwamba, usajili wa TIN unafanyika kwa kutumia taarifa za NIN. Aidha, kila mwenye TIN ambaye alisajiliwa awali kwa kutumia vitambulisho tofauti na kitambulisho cha NIDA, anatakiwa kuhuisha taarifa zake za TIN ziendane na taarifa zilizopo kwenye NIN.

Ili zoezi la uhuishwaji wa taarifa hizi lifanyike kwa urahisi na wepesi, inashauriwa kwamba kila mwenye TIN ambayo bado haijahuishwa, kufika katika ofisi za TRA zilizo karibu naye akiwa na Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN) ili taarifa zake ziweze kuhakikiwa na kuhuishwa. Kwa wale wenye NIN lakini hawana TIN, wanaweza kufanya usajili wa TIN kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Ikumbukwe kwamba huduma zote za utoaji wa TIN ni bure na rahisi. Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo Karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| **Tovuti** | : | **www.tra.go.tz** |
| **Namba za Simu bila malipo** | : | **0800 750 075 au 0800 780 078 au 0800 110016** |
| **WhatsApp** | : | **0744 23 33 33** |
| **Barua pepe** | : | **huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz** |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**
**TRA MAKAO MAKUU**

217316402



# Ubovu barabara wasababisha hasara ya bil.2/- kwa wakulima

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WAKULIMA wanaozalisha maembe ya kisasa katika Kata ya Kwedihuti, Kijiji cha Mvungwe, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga, wamesema wanapata hasara ya zaidi ya Sh. bilioni mbili kila mwaka kutokana na kushindwa kufikisha mazao yao sokoni.

Wamesema ubovu wa barabara ndiyo kikwazo kikuu cha wao kushindwa kusafirisha bidhaa zao kwenda sokoni.

Akizungumzia hali hiyo, mmoja wa wakulima hao Hassan Omar, alisema hasara anayopata kutokana na sababu hizo ni kupoteza Sh. milioni 20 kutokana na mazao yake kuozea shambani, kwa kukosa wanunuzi wanaodai malori yao ya mizigo hayawezi kupita kwenye barabara ya Kwedihuti/Mvungwe hadi Songe.

Zuhura Kalabaka, alisema licha ya kuwapo kwa barabara lakini anashangazwa na hatua ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), kutowajibika kuifanyia matengenezo.

Bakari Mussa, alisema hawanufaiki na chochote kwenye mradi huo zaidi ya kuendelea na umasikini, kwa kuwa mazao yao hayana bei.

Alipoulizwa Mwenyekiti wa Ushirika huo, Mohamed Magenda kuhusu madai hayo, alisema bei ya shillingi mia moja kwa embe wanayouza ni hasara kubwa ikilinganishwa gharama za uendeshaji.

Mradi huo unaoendeshwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, kwa ufadhili wa Shirika la World Vision Tanzania, kupitia Mradi wa AP Mgera, ambao hivi sasa uko katika hali mbaya kutokana na kukosa huduma muhimu kama maji kwa ajili ya umwagiliaji, barabara na viuatilifu. Meneja wa Worldvision-AP Mgera, Modest Kessy, alisema awali walikuwa wafadhili wa mradi huo, baada ya kumaliza muda wa mradi walikabidhi majukumu kwa halmashauri kama wasimamizi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, Gracian Makota, alipoulizwa kuhusiana na malalamiko hayo alisema: "Mradi huo siyo wa faida kwa halmashauri, ni kwa ajili ya kuwaongezea uchumi wananchi na uendeshaji wake upo mikononi mwa uongozi wao". Alisema: "Lakini suala la soko wanatakiwa walisake lilipo, lakini kuhusu barabara tutawasiliana na TARURA ili washughulikie tatizo hilo na kuwafungulia njia wananchi hao kufikia malengo yao ya kiuchumi".

Meneja wa TARURA wa Wilaya ya Kilindi, Martin Mwashambwa, alipoulizwa kuhusu malalamiko hayo aliahidi kufuatilia na kuona namna ya kuiondoa kero hiyo kwa wakati ili wakulima hao na wengine wapate huduma inayostahili.

# Vijiji kando ya Mlima Kilimanjaro kupanda miti 150,000

**Na Mary Mosha,** ROMBO

VIJIJI 20 kati ya 94 vinavyoizunguka Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro vinatarajia kupanda miti 150,000 katika maeneo yao wakati wa msimu wa mvua za masika ili kuisaidia hifadhi hiyo kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira.

Akizungumzia mpango huo wa pamoja, Kaimu Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa KINAPA, Imani Kikoti, alisema mpango huo unalenga kupunguza shughuli za binadamu hasa uvunaji wa kuni, urinaji wa asali na kilimo, ambavyo vimekuwa sehemu ya visababishi vya moto katika hifadhi hiyo.

Alisema ili kulinda ikolojia na bioanuai ya hifadhi hiyo KINAPA imeandaa kitalu chenye miche 300 ya miti, ambayo wananchi wa vijiji hivyo watawasilisha ombi na aina ya miti wanayoitaka kwa ajili ya kupandwa kuzunguka hifadhi hiyo.

"Kati ya wilaya zinazoizunguka KINAPA, Wilaya ya Hai, ndiyo yenye vijiji vingi vyenye shughuli za binadamu hatarishi ambazo zimekuwa zikisababisha moto mara kwa mara. Sasa kuelekea maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge, Machi 16 mwaka 1974, tunataka kuja na mpango mahususi wa kulinda ikolojia na bioanuai kwa kushirikisha vijiji jirani, alisema na kuongeza:

"Tunatoa rai kwa jamii kuwa makini na usimamizi wa moto wanayoianzisha wakati wa uandaaji wa mashamba ya kilimo hivi sasa, kwa kuwa unaharibu mazingira kwa kiasi kikubwa." Alisema.

Alisema endapo matukio ya moto yasipodhibitiwa yataendelea kumaliza uoto wa alisi uliobakia na madhara ya mabadiliko ya tabianchi yanaweza kuongezeka, ikiwamo kusababisha kukauka kwa vyanzo vya maji, ongezeko la joto na madhara ya ikolojia.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, akitoa maelekezo kwa kuagiza taasisi zote zilizoko mkoani humo kuhakikisha zinapanda miti, hasa katika shule za msingi na sekondari, ofisi ya kjiji, kata, tarafa, wilaya na mkoa.

Aidha, baadhi ya wadau wa utalii wanaoshiriki mpango huo wa upandaji wa miti, akiwamo Ofisa Masoko wa Kampuni ya Uendeshaji wa Utalii ya ZARA Tours, Nancy Ngotea, alisema suala la upandaji miti kwao ni lazima, siyo hiari katika kuhakikisha wararudisha uoto wa asili.



Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe De Boer (katikati waliokaa), akiwa pamoja na wadau kutoka serikali na taasisi mbalimbali wakati wa uzinduzi wa programu iliyolenga kuinua na kukuza kilimo cha mboga katika mikoa ya Kaskazini uliofanyika mkoani Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Naibu Waziri achukizwa viongozi wa wilaya kuwatishia wananchi

**Na Allan Isack,** LONGIDO

NAIBU Waziri wa Madini, Dk. Stephen Kiruswa, amesikitishwa na vitendo vya baadhi ya viongozi wa Wilaya ya Longido mkoani Arusha, kudaiwa kuwatisha wananchi wanapoulizia juu ya hatima ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Olmolok.

Amesema jambo hilo halikubaliki na wanaotakiwa kutoa majibu hawapaswi kuwadhihaki wananchi.

Dk. Kiruswa ambaye ni Mbunge wa Longido, alisema amepokea taarifa kutoka kwa wananchi wake kwamba wanatishiwa na viongozi wanapowahoji kuhusu kukamilika kwa mradi huo, wakitishiwa kukamatwa na kufunguliwa mashtaka.

Alieleza hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea Kata ya Olmolok na kukagua mradi huo ambao ulipaswa kukamilika Juni mwaka jana, baada ya serikali kutoa Sh. milioni 903 za ujenzi.

"Kutokana na haya yanayoendelea, nawapa RUWASA (Wakala wa Maji Vijijini), wiki tatu maji yatoke na wananchi wafanye shughuli nyingine za maendeleo siyo kusaka maji umbali mrefu, wakati mradi wao ulishatengewa fedha,"alisema.


Alisema kutokana na madai hayo ya vitisho, alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Longido kuchunguza, kisha kuwashughulikia kwa kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria wanaowatishia wananchi hao.

Alisema serikali ilitenga Sh. milioni 903 kwa ajili ya mradi wa maji katika kata hiyo na kata nyingine za jirani lakini hadi sasa mkandarasi amelipwa Sh.milioni 300.

Alisema hafahamu fedha zilizobaki zinafanyia shughuli gani, kwa kuwa hadi sasa mradi umechelewa na haujakamilika kwamba ulipaswa kukamilika tangu mwaka jana.

Akijibu malalamiko hayo, Meneja wa RUWASA wa Wilaya ya Longido, Petro Nyerere, alisema kuchelewa kukamilika kwa mradi kumetokana na matatizo mengi aliyopata mkandarasi ikiwamo usafiri wa kusafirisha vifaa kutoka makao makuu ya wilaya na kuchelewa kwa fedha kumfikia mkandarasi kwa wakati.

Kwa mujibu wa Nyerere, baada ya Mbunge wa Jimbo kukubali kutoa usafiri wake kusafirisha vifaa vya ujenzi na kusimamia malipo ya mkandarasi, kazi hiyo huenda ikakamilikaa ndani ya wiki tatu alizozitoa.





## DC awakumbusha wanawake wajibu wao katika malezi

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WANAWAKE wametakiwa kujua majukumu yao katika malezi ili kudhibiti mmomonyoko wa maadili pamoja na kudhibiti vitendo vya unyanyasaji kingono, ambavyo vimeendelea kushamiri. Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani na kusema kuwa wazazi wanajukumu la kushiriki katika malezi ya watoto.

Alisema katika miaka hii mmomonyoko wa maadili umekuwa ukitishia mustakabari wa malezi kwa watoto, hali inayosababishwa na idadi kubwa ya wazazi kujikita zaidi katika shughuli za kiuchumi na kusahau wajibu wao.

Aidha, aliongeza kuwa siku hizi wazazi wamejisahau na hawatimizi majukumu yao kama mama, hawafuatilii mienendo ya maisha ya watoto wao. Ofisa Utumishi Wilaya ya Sengerema, Christina Bunini, alisema jukumu la kulea mtoto ni la wazazi na siyo kuwapeleka watoto shuleni wakiwa wadogo na hawajajitambua hali inayowafanya watoto hao kwenda kuishi shuleni na kukosa malezi ya wazazi wao.

Alisema wanawake walio wengi wanashindwa kusimamia majukumu yao, kwamba unakuta mtoto anafanya mambo mabaya ambayo hayafai katika jamii, akiulizwa anasema aliona kwenye simu.

Hivyo, aliwataka wazazi kuacha kuwapa simu watoto kwani zinaharibu maadili yao.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Sengerema, Yusia Mwambembe, alisema wataendelea kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya mtandao kwa kinamama ili wakawafundishe watoto na kuwaelimisha.

Lightness Urassa ambaye ni mwalimu alisema ma anawajibu wa kutoa elimu juu ya madhara ya kutumia mitandao kwa watoto ambao bado hawajajitambua ili kuwaokoa katika wimbi la mmomonyoko wa maadili.

# H/shauri yatoa mbegu za mtama kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imetoa bure mbegu za mtama kilo 1,000 katika shule za msingi na sekondari ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, pamoja na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara shuleni.

Pia imetoa pembejeo za kilimo kwa wakulima vijana 71 wenye uwezo wa kulima hekari tano za mazao ya chakula na biashara kutoka katika kata hizo, ili kuongeza uzalishaji na kujikwamua kiuchumi kupitia kilimo.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Ofisa Kilimo ambaye pia ni Ofisa Ushirika wa Halmashauri hiyo, Adronic Kamugisha, wakati wa ugawaji wa pikipiki 25 kwa maofisa ugani wa kata zilizotolewa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo.

Alisema tangu umeanza utaratibu wa ugawaji wa pembejeo mwaka wa fedha 2018/2019 mpaka sasa wakulima vijana 172 wameshanufaika, huku Sh. milioni 115.7 zilikitumika kugharamia pembejeo hizo.

Alisema wametoa mbegu za mtama na alizeti katika shule za msingi na sekondari zenye maeneo ya kilimo, kwamba maofisa ugani hao watazitumia pikipiki hizo kuzitembelea shule na kuhakikisha wanapata ushauri wa kulima kisasa kulingana na maeneo yao na namna ya kuvuna baada ya mazao kukomaa shambani.

Kaimu Mkurugenzi ambaye ni Mwanasheria wa Halmashauri hiyo, Stephen Magalla alisema, serikali imeendelea kuboresha maslahi ya watumishi kwa kuwapatia vitendea kazi na pikipiki hizo zinatakiwa kutumika katika matumizi yaliyopangwa na siyo vinginevyo.

Alisema hivi karibuni walinunua pikipiki 19 kwa kutumia fedha za mapato ya ndani, kati ya hizo, sita walizotoa kwa baadhi ya maofisa ugani, tano kwa watendaji wa kata na nane kwa maofisa maendeleo ya jamii.

Akizungumza kwa niaba ya maofisa ugani, Ofisa Ugani wa Kata ya Kilago, Renord Uloto alisema pikipiki hizo zitawasaidia kuwafikia wakulima.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita alisema, halmashauri hiyo ina hekta 62,422.7 zilizotumika katika kilimo cha mpunga, pamba, karanga, dengu, mahindi, alizeti na mazao mengine na serikali imekuwa ikifanya jitihada kuhakikisha kilimo kinakuwa kwa asilima 10 ifikapo mwaka 2030.




Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mwingilo wilayani Geita, wakifurahia zawadi za taulo za kike walizokabidhiwa na wanawake wafanyakazi wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu kama sehemu ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji wadogo wa madini walipa kodi mil.173.7/-

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya dhahabu mgodi wa Mwakitolyo namba 5 uliopo wilayani Shinyanga, wamelipa kodi ya Sh.milioni 173.7 zilizotokana na mapato ya mgodini.

Walieleza hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara uliokuwa na dhumuni la kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya uzalishaji wa madini ya dhahabu, pamoja na kutangaza mikakati ambayo wamejiwekea, kusaidia shughuli za kijamii, kupitia umoja wao wa vitalu vya uchenjuaji wa madini.

Meneja wa Vitalu katika mgodi huo, Leonard Waziri, akisoma taarifa ya uzalishaji madini kwa mwaka 2022 alisema kwa kipindi hicho wamezalisha dhahabu gramu 18,507.8 yenye thamani ya Sh.bilioni 2.3. Alisema kupitia uzalishaji huo wameweza kulipa mapato ya serikalini Sh. milioni 165, na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Sh. milioni 7.7, huku wakichangia pia shughuli za kijamii kwa kujenga kituo cha polisi, madarasa kwa shule za msingi na sekondari, pamoja na Ofisi ya Mwenyekiti wa Kijiji na Soko la Madini.

Mhasibu wa umoja wa mgodi huo, Janeth Ngangula, akisoma taarifa ya fedha alisema kulingana na matumizi waliyoyafanya mpaka sasa wamebakiwa na Sh.milioni 213, kwamba kwa mwaka huu wamepanga kununua gari la kubebea wagonjwa, ikiwa ni sehemu ya kusaidia jamii.

Mwenyekiti wa wachimbaji wadogo katika mgodi huo, Mathew Tune, alisema lengo la kuitisha mkutano huo ni kutekeleza sera ya ukweli na uwazi na kuondoa migogoro isiyo na tija ya madai ya fedha kuliwa.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Edward Ngelela, alisema kusoma mapato na matumizi, ni wajibu wa kila sekta katika jamii ikiwa ni sehemu ya kuweka uwazi katika utendaji kazi wao.

Aidha alitoa wito kwa viongozi wote wilayani humo kuanza ngazi ya vitongoji kujenga utaratibu wa kusomea wananchi wao mapato na matumizi ikiwa ni pamoja na kubainisha shughuli zilizofanyika ili kuweka uwazi kwa jamii.

Nipashe
Spotika



HALAAND UKURASA 14




DE BRUYNE

# WACHEZAJI WA5 WANAOTUMIA MIGUU YOTE KWA UBORA SAWA

**LONDON,** England

KATIKA mpira wa miguu mchezaji kutumia miguu yote kwa ustadi na usahihi ni nadra sana. Ni ubora unaoweza kumpa mchezaji faida kubwa dhidi ya wapinzani wake.

Mchezaji mwenye uwezo wa kutumia miguu yote miwili anaweza kubadili mwelekeo wa kucheza chenga kwa urahisi, kupiga mashuti kutoka pembeni na nafasi tofauti na kupasisha mpira kwa usahihi na kasi akitumia mguu wowote.

Ustadi huu unaweza kuleta mkanganyiko kwa mabeki ambao huenda wasijue mchezaji atapita njia gani au atatumia mguu gani. Mchezaji wa miguu miwili pia anaweza kuwa fiti zaidi na kubadilika kwa nafasi tofauti uwanjani.

Kwa mfano, winga ambaye yuko na furaha kutumia miguu yote miwili anaweza kuwa na ufanisi sawa katika pande zote za uwanja, hivyo kufanya iwe vigumu kwa mabeki kuziweka alama. Kwa ujumla, uchezaji wa miguu miwili ni ustadi unaothaminiwa sana katika soka ambao unaweza kumfanya mchezaji kuwa bora zaidi na wa thamani kwa timu yake.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano bora wenye uwezo wa kutumia miguu yote miwili dimbani, haya sasa...

**#5 Son Heung-Min (Tottenham Hotspur)**

Son Heung-Min ni mmoja wa washambuliaji bora wa kizazi chake. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini, amekuwa mtu muhimu pale Tottenham Hotspur tangu ajiunge na klabu hiyo mwaka 2015. Alishinda kwa pamoja Kiatu cha Dhahabu cha ufungaji bora wa Ligi Kuu England na Mohamed Salah.

Ni mchezaji mahiri na hodari ambaye anasifika kwa ustadi wake wa kucheza chenga na uwezo wa kupata bao kutoka kwa masafa marefu. Ana wepesi sawa kwa miguu yake yote miwili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 msimu huu hajawa kwenye kiwango chake bora, amefunga mabao tisa na kutoa asisti tatu katika mechi 33 alizocheza kwenye mashindano yote akiwa na Tottenham kufikia sasa msimu huu.

**#4 Sergej MilinkovićSavić (Lazio)**

Kiungo wa kati wa Lazio, Sergej MilinkovićSavić anajulikana kwa sifa zake za kuvutia za kimwili na uwezo wa kiufundi. Ni kiungo mrefu na mwenye nguvu ambaye yuko vizuri kucheza kama kiungo mkabaji na kiungo mshambuliaji.

Zaidi ya hayo, ana uwezo wa kutumia miguu yote miwili, ambayo ina maana kwamba anaweza kutumia miguu yote kwa usawa, na kumfanya asitabirike kwa wapinzani wake.

Amefunga mabao sita na kutoa pasi nane za mabao katika mechi 31 alizocheza kwenye michuano yote akiwa na Lazio hadi sasa msimu huu.

**#3 Neymar Jr (Paris Saint-Germain)**

Neymar Jr. alikuwa katika kiwango kizuri mwanzoni mwa msimu. Mchezaji huyo wa Brazil anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji mahiri wa kizazi chake. Uwezo na ubunifu ni vitu muhimu sana kwake.

Ustadi wa Neymar wa kupiga chenga unazingatiwa sana, na ana uwezo wa kuwashinda mabeki kwa urahisi. Sifa nyingine muhimu ya Neymar ni kuwa na uwezo wa kutumia miguu yote miwili. Uwezo huu unamfanya kuwa mgumu kutabiri na kumkaba, kwani anaweza kubadilisha mwelekeo haraka au kupiga shuti kwa mguu wowote.

Katika mechi 29 za michuano yote aliyoichezea Paris Saint-Germain hadi sasa, amefunga mabao 18 na kutoa asisti 17.

**#2 Kevin De Bruyne (Manchester City)**

Kevin De Bruyne anasifika kwa umahiri wake wa ufundi na anatajwa sana kuwa kiungo mshambuliaji bora wa kizazi chake. Ana udhibiti bora wa mpira, ustadi wake wa kupiga pasi na ni mahiri katika kutengeneza nafasi za kufunga mabao kwa wachezaji wenzake.

De Bruyne ni mchezaji wa miguu yote miwili. Anaweza kupiga pasi, kupiga shuti na hata kupiga chenga kwa miguu yote miwili na hii inafanya kuwa vigumu kwa mabeki kutarajia hatua yake inayofuata. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ana uwezo wa kupiga shuti akiwa katika nafasi mbalimbali.

Ingawa anapendelea kutumia zaidi mguu wake wa kulia, De Bruyne amefunga mara nyingi kwa kutumia mguu wake wa kushoto. Katika mechi 32 katika michuano yote aliyoichezea Manchester City kufikia sasa msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amefunga mabao matano na kutoa asisti 18.

**#1 Ousmane Dembele (Barcelona)**

Winga wa Barcelona, Ousmane Dembele, anasifika kwa uwezo wake wa kipekee wa kiufundi kwenye mpira. Ni fowadi hodari ambaye anaweza kucheza kama winga ama mshambuliaji. Ubora wa kuvutia zaidi wa Dembele ni uwezo wake wa kupiga chenga kwa miguu yote miwili, jambo linalomwezesha kuwapita mabeki kwa urahisi.

Pia ni mpigaji sahihi wa mpira na anaweza kutoa krosi kwa usahihi kwa kutumia miguu yote miwili. Zaidi ya hayo, Dembele ana mbinu bora kwa miguu yote, inayomruhusu kufunga mabao kutoka pembe tofauti.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, amefunga mabao nane na kutoa asisti saba katika mechi 28 kwenye michuano yote hadi sasa msimu huu akiwa na Barcelona.

## ISIKUPITE

BAO alilofunga Kylian Mbappe wakati wakishinda 2-1 dhidi ya Brest juzi, lilikuwa la 3,000 kwa PSG kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, lakini kubwa zaidi ni Lionel Messi kuweka rekodi yake binafsi, kwani alitoa pasi yake ya mwisho ('assists') ya 300 kwa klabu katika maisha yake ya soka, jambo ambalo hakuna mchezaji mwingine yeyote aliyeweza kuifikia.



# WACHEZAJI 10 WENYE TUZO NYINGI BINAFSI


LIONEL MESSI

**LONDON,** England

MCHEZO wa soka ni kuhusu mataji na tuzo. Katika ngazi ya kimataifa na klabu, timu ziko kwenye vita ya mara kwa mara ya kuwania ukuu ambao huamuliwa kwa heshima wanazoshinda. Ingawa mpira wa miguu ni mchezo wa timu, tuzo za mtu binafsi bado ni muhimu. Tuzo kama vile Ballon d'Or na Mchezaji Bora wa Mwaka wa Fifa bado ndizo za kifahari kuliko zote.

Kumbuka: Tuzo zinazozingatiwa katika orodha hii zile za juu za Ulaya na Fifa, ambazo ni pamoja na Ballon d'Or, Mchezaji Bora wa Mwaka wa Fifa, Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya/Kiatu cha Dhahabu Mfungaji Bora kwenye Ligi na Tuzo ya Fifa Puskas.

Hapa tunawaangalia wanasoka 10 wenye tuzo nyingi zaidi binafsi katika soka duniani, twende sasa...

**#10 Ronaldinho (Brazil) - 3**

Nyota wa zamani wa Barcelona na gwiji wa Brazil yupo nafasi ya 10. Ronaldinho anajulikana kwa kucheza chenga na kudhibiti vema mpira. Kwa haiba yake na tabia yake ya utulivu, alishinda mioyo ya wafuasi wengi, na wanasoka wenzake. Kiungo huyu mshambuliaji, pia alicheza kama mshambuliaji au winga.

Katika ubora wake, hakukuwa na wachezaji wengi ambao wangeweza kuendana na kiwango chake. Mara nyingi angeamua mechi peke yake. Katika maisha yake yote ya soka, Mbrazil huyo aliyependa kutabasamu, ameshinda tuzo tatu kuu binafsi. Ametunukiwa tuzo ya Ballon d'Or mara moja, amepokea tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia wa Fifa mara mbili.

Katika kipindi chake cha miaka mitano Barcelona kuanzia 2003 hadi 2008, alishinda mataji mengi yakiwamo mataji mawili ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga (2004-05 na 2005-06) na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2005-06. Akiwa na AC Milan, alitwaa taji lake la pekee na la Milan la Serie A msimu wa 2010-11.

Kwa upande wa kimataifa, alishinda Copa America akiwa na Brazil mwaka 1999. Mataji mengine mawili ni Kombe la Dunia la FIFA la 2002 na Kombe la Shirikisho la FIFA la 2005.

**#9 Gerd Muller (Ujerumani) - 3**

Akiwa na Ballon d'Or na tuzo mbili za Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora Ulaya, gwiji huyo wa Bayern Munich na Ujerumani, Gerd Muller anashika nafasi ya tisa. Akiwa na mabao 721 kwa jina lake, Muller mara nyingi huchukuliwa kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi wa wakati wote.

Mshambuliaji mahiri aliyesifika kwa umaliziaji wake, haswa ndani na karibu na eneo la yadi sita, alikuwa jinamizi kwa walinzi pinzani. Muller alitumia muda mwingi wa uchezaji wake pale Bayern Munich na alifunga mabao 564 katika mechi 605. Katika mchakato huo, alishinda mataji manne ya Bundesliga (1968-69, 1971-72, 1972-73, 1973-74) na alisaidia sana katika Kombe la Ulaya mara tatu kutoka 1974 hadi 1976.

Pia, hakuwa mzembe katika hatua ya kimataifa. Akiwa amefunga mabao 68 kwenye michezo 62 ya Ujerumani, alishinda mataji mawili ya kimataifa. La kwanza ni Euro 1972, na miaka miwili baadaye, akashinda Kombe la Dunia la FIFA la 1974.

**#8 Eusebio (Ureno) - 3**

Nafasi ya nane yupo Eusebio, pia anajulikana kama Black Panther. Akiwa na mabao 733 katika mechi 745, Black Panther ameandika jina lake katika historia. Alijulikana kwa kasi yake, ufundi, na mashuti makali ya mguu wa kulia, na kumfanya kuwa mfungaji hodari. Akiwa na mabao 473 katika mechi 430, ndiye mfungaji wa muda wote wa Klabu ya SL Benfica.

Mnamo 1965, alikuwa mchezaji wa kwanza mzaliwa wa Afrika kushinda Ballon d'Or. Alishinda Kiatu cha kwanza cha Dhahabu cha Ulaya mwaka 1968 na akafanya hivyo tena mwaka 1973.

Alifurahia mafanikio makubwa akiwa na Benfica, hivyo kushinda mataji 11 ya Primera Liga (Ligi Kuu ya Ureno) na Kombe la Ulaya katika msimu wa 1961-62. Mabao yake 41 katika mechi 64 za kimataifa yanamfanya kuwa mfungaji bora wa pili wa wakati wote wa Ureno.

**#7 Michel Platini (Ufaransa) - 3**

Huyu ni Rais wa zamani wa UEFA na mwanasoka wa Ufaransa, Michel Platini. Mara nyingi akizingatiwa kama mmoja wa wanasoka bora wa kizazi chake, nahodha huyo wa Ufaransa, alishinda Ballon d'Or tatu mfululizo kutoka 1983 hadi 1985. Licha ya kucheza kama mchezaji wa hali ya juu, alikuwa mfungaji mahiri pia. Akiwa amefunga mabao 353 katika mechi 652 kwa klabu na nchi, mara nyingi anashika nafasi ya kati ya alama za juu katika historia ya mchezo huo.



Akiwa amecheza soka kwa zaidi ya miaka 15, gwiji huyo wa zamani wa Ufaransa na Juventus alishinda tuzo kadhaa katika ngazi ya klabu na kimataifa. Alishinda Ligue 1 ya msimu wa 1980-81 akiwa na Saint-Etienne na mataji mawili ya Serie A akiwa na Juventus msimu wa 1983-84 na 1984-85. Akiwa na 'Bibi Mzee' (Juve), pia alishinda Kombe la Ulaya msimu wa 1984-85.

**#6 Johan Cruyff (Uholanzi) - 3**

Gwiji wa Uholanzi, Johan Cruyff anashika nafasi ya sita. Mwanasoka mwenye akili na kipaji cha kiufundi, mara nyingi hujumuishwa miongoni mwa wachezaji wakubwa katika historia ya soka. Alichukuwa jukumu kubwa katika kuinua soka la Uholanzi kutoka kusikojulikana mwishoni mwa miaka ya 1960 hadi kuwa na nguvu kubwa katika soka la dunia.

Cruyff alifunga mabao 416 kwa klabu na nchi katika mechi 716. Alishinda mataji tisa ya Eredivisie (Ligi Kuu Uholanzi), nane akiwa na Ajax na lililosalia akiwa na Feyenoord. Akiwa na Ajax, alishinda Kombe la Ulaya mara tatu mfululizo kuanzia mwaka 1971 hadi 1973. Kwa mafanikio yake akiwa na klabu ya Amsterdam, alitunukiwa tuzo ya Ballon d'Or mara tatu, mwaka 1971, 1973 na 1974.

Mbali na kuwa mchezaji bora, alikuwa kocha mzuri pia. Akiwa mmoja wa watu mashuhuri katika historia ya soka, mtindo wake wa uchezaji umeigwa na makocha wengi na wachezaji kadhaa, wakiwamo Arrigo Sacchi, Sir Alex Ferguson, Pep Guardiola na wengine wengi.

**#5 Zinedine Zidane (Ufaransa) - 4**

Akiwa na tuzo nne za binafsi kwa jina lake, Zinedine Zidane anashika nafasi ya tano. Mmoja wa viungo bora kuwahi kuupamba mchezo huo. Zidane alijulikana kwa uwezo wake wa kumiliki mpira na kutoa pasi za hali ya juu, ni mfungaji hodari, ana mabao 156 katika mechi 792 akiwa na klabu na nchi.

Gwiji huyo wa zamani wa Juventus na Real Madrid, alishinda Serie A msimu wa 1996-97 na 1997-98 na Supercoppa Italiana mwaka 1997 akiwa na klabu hiyo ya Turin. Mwaka 1998 ulikuwa mzuri kwa ushindi wa kwanza wa Kombe la Dunia kwa Ufaransa katika ardhi yao na kumfanya apate tuzo yake ya kwanza ya Ballon d'Or na ya kwanza kati ya tatu za mchezaji bora wa mwaka wa FIFA mwaka 1998. Alifunga mabao mawili katika fainali hiyo ya Kombe la Dunia. Tuzo nyingine ya Mchezaji Bora wa Dunia wa FIFA ilifuata 2000 alipoisaidia Ufaransa kutwaa taji la Euro 2000.

Hata hivyo, ilikuwa Real Madrid, ambapo alifurahia mafanikio ya Ulaya. Katika msimu wake wa kwanza akiwa na klabu hiyo ya Hispania, alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2001-02. Katika msimu uliofuata, alishinda LaLiga ambayo ilimfikisha kwenye tuzo hii ya tatu ya Mwanasoka Bora wa Dunia wa FIFA mwaka 2003. Kwa jumla, alishinda mataji sita akiwa na 'Los Blancos' hao na alimaliza maisha yake ya klabu akiwa na Madrid mwaka 2006.

**#4 Marco van Basten (Uholanzi) - 5**

Nafasi ya nne ni ya Marco van Basten. Mshambuliaji mahiri anayejulikana kwa udhibiti wake wa karibu wa mpira, akili ya kushambulia, na mipira ya kuvutia na ni mmoja wa wafungaji bora wa soka akiwa amefunga mabao 301 katika mechi 431. Hata hivyo, jeraha la kifundo cha mguu lilimlazimu kustaafu mapema akiwa na umri wa miaka 28.

Licha ya hayo, bado anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora wa wakati wake. Akiwa na Ajax, alishinda mataji matatu ya Eredivisie (Ligi Kuu Uholanzi) msimu wa 1981-82, 1982-83 na 1984-85. Kwa kufunga mabao 37 katika Eredivisie msimu wa 1985-86, alishinda Kiatu chake cha kwanza na pekee cha Dhahabu cha Ulaya.

Hata hivyo, alijitengenezea jina lake katika timu kubwa ya Arrigo Sacchi ya AC Milan mwishoni mwa miaka ya 80' na mapema miaka ya 90'. Alishinda tuzo zake zote tatu za Ballon d'Or akiwa na wababe hao wa Italia. Mbali na hayo, Mchezaji Bora wa Dunia wa FIFA wa mwaka 1992, alishinda Serie A mara tatu (1987-88, 1991-92 na 1992-93) na Kombe la Ulaya msimu wa 1988-89 na 1989 -1990. Akiwa na Uholanzi, van Basten alishinda Euro ya mwaka 1988.

**#3 Ronaldo Nazario (Brazil) - 6**

Ronaldo Nazario, anayejulikana pia kama Fenomeno, anashika nafasi ya tatu kati ya wachezaji walio na tuzo nyingi binafsi. Kwa mbinu yake, chenga, na umaliziaji wa kitaalamu, alikuwa mshambuliaji kamili na alibadilisha mtazamo wa mshambuliaji kuwa wa kisasa. Akiwa katika ubora wake, alichezea klabu nyingi za juu zikiwamo Cruzeiro, PSV, Barcelona, Inter Milan na Real Madrid.

Mabao yake 414 katika mechi 616 kwa klabu na nchi, yanatosha kumweka katika kundi la washambuliaji wakubwa. Wakati wa msimu wake mmoja pale Barcelona, alikuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kushinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia wa FIFA mwaka wa 1996 akiwa na umri wa miaka 20. Mwaka uliofuata alishinda Ballon d'Or na Mchezaji Bora wa Dunia wa FIFA wa mwaka. Pia akiwa na Wakatalunya hao, alitwaa kiatu chake cha kwanza na pekee cha dhahabu cha Ulaya kwa kufunga mabao 34 msimu wa 1996-97 wa LaLiga. Alishinda mataji yake mawili pekee ya ligi akiwa na Real Madrid katika msimu wa 2002-03 na 2006-07.

Ronaldo alishinda mataji matatu ya kimataifa katika maisha yake ya soka. Sehemu ya kikosi kilichoshinda Kombe la Dunia la FIFA la 1994, alishinda Copa America mara mbili mnamo mwaka 1997 na 1999. Wakati mzuri zaidi wa maisha yake ulifika kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2002. Akiwa amekaa nje ya uwanja kwa miaka miwili, alirejea kwa kishindo na kufunga mabao nane na kuipa Brazil Kombe la Dunia la tano.

**#2 Cristiano Ronaldo (Ureno) - 24**

Akiwa na tuzo 29 kwa jina lake, Cristiano Ronaldo ni mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote. Akiwa na jumla ya mabao 679 kwa klabu na nchi katika mechi 952, ndiye mfungaji bora anayecheza soka la kimataifa.

Safari hiyo ilianza mwaka 2008 aliposhinda tuzo yake ya kwanza ya Ballon d'Or na FIFA ya Mwanasoka Bora wa Mwaka wa Dunia mwaka wa 2008 baada ya kuiongoza Manchester United kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa mara mbili msimu wa 2007-08. Pia alishinda Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya msimu huo, akifunga mabao 31 kwenye Ligi Kuu. Baadaye mwaka wa 2009, alishinda tuzo ya FIFA Puskas. Kuanzia 2006-09, alishinda mataji matatu mfululizo ya Ligi Kuu. Kwa jumla, alipata mataji tisa katika kipindi chake cha miaka sita pale Manchester.

FIFA Ballon d'Or/Ballon d'Or: 2008, 2013, 2014, 2016, 2017 (mara 5)

Mchezaji Bora wa Dunia wa FIFA: 2008, 2016, 2017 (mara 3)

Tuzo Bora Zaidi Maalum ya FIFA kwa Mafanikio Bora: 2021 (mara 1)

Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya: 2007-08, 2010-11, 2013-14, 2014-15 (mara 4)

Mpira wa Dhahabu wa Kombe la Dunia la Klabu ya FIFA: 2016 (mara 1)

Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya: 2020 (mara 1)

Mchezaji Bora wa Ligi Kuu ya England: 2006-07, 2007-08 (mara 2)

Mchezaji Bora wa LaLiga: 2013-14 (mara 1)

Mwanasoka Bora wa Mwaka wa Serie A: 2019, 2020 (mara 2)

Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu: 2007-08 (mara 1)

Mfungaji Bora LaLiga, Pichichi: 2010-11, 2013-14, 2014-15 (mara 3)

**#1 Lionel Messi (Argentina) - 27**

Lionel Messi anashika nafasi ya kwanza katika orodha ya wanasoka wenye tuzo nyingi binafsi. Akizingatiwa na wachezaji wengi, mashabiki, wachambuzi, kama mchezaji bora zaidi wa wakati wote, amefunga mabao 650 katika mechi 799 za klabu na nchi. Kwa akili yake ya soka, ujuzi wa kiufundi, ustadi wa kucheza, Muargentina huyo amekuwa sura ya mwanasoka kamili.

Ballon d'Or/FIFA Ballon d'Or: 2009, 2010, 2011, 2012, 2015, 2019, 2021 (mara 7)

Mchezaji Bora wa Dunia wa FIFA: 2009, 2019, 2022 (mara 3)

Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya: 2009-10, 2011-12, 2012-13, 2016-17, 2017-18, 2018-19 (mara 6)

Mpira wa Dhahabu wa Kombe la Dunia la FIFA: 2014, 2022(mara 2)

Mpira wa Dhahabu wa Kombe la Dunia la Klabu ya FIFA: 2009, 2011 (mara 2)

Mchezaji Bora wa Copa America: 2015, 2021 (mara 2)

Mfungaji Bora wa Copa America: 2021 (mara 1)

Mchezaji Bora wa LaLiga: 2008-09, 2009-10, 2010-11, 2011-12, 2012-13, 2014-15(mara 6)

Mfungaji bora LaLiga, Pichichii: 2009-10, 2011-12, 2012-13, 2016-17, 2017-18, 2018-19, 2019-20, 2020-21(mara 8)

## Nukuu

"Ni maalum sana [kuvunja rekodi] - siku zote nimekuwa nikiifukuzia rekodi hiyo - nitaenda nyumbani na kusherehekea na familia," **Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, baada ya kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa 'Wekundu' hao kwenye Ligi Kuu England akiwa amefunga mabao 129 na kuipiku ile ya Robbie Fowler, ambaye enzi zake alicheka na nyavu mara 128.**



"Kwangu mimi ni jambo la muhimu sana na ambalo hatuzungumzi vya kutosha ni taaluma yake. Kila mara tunazungumza juu ya mabao yake, kasi yake, lakini ni mtu anayefanya kazi, anayekuja mazoezini mapema, ambaye huwa uwanjani kila wakati ambaye daima anataka kujifunza na kujaribu kwenda mbele zaidi. Unapowatazama mabosi wawili waliomtangulia, [Cristiano] Ronaldo na [Lionel] Messi, ni kitu kimoja. Ndiyo maana nilimwita mrithi kwa sababu ndiye anayenifuata na hilo liko wazi," **Nyota wa zamani wa Ufaransa, Thierry Henry, akimtaja Kylian Mbappe kama mrithi wa Messi na Ronaldo katika soka la dunia.**



"Ikiwa PSG wanataka kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa, kuna makocha wawili ambao wanapaswa kuwafuata. Mmoja ni Diego Simeone, kwa sababu nadhani ukimpatia zana za kazi kwa ulinzi watakuwa wazuri sana, vipaji walivyonavyo unaweza karibu kusema 'unajua nini, nenda kafanye unachohitaji kufanya. Na mwingine ni Jose Mourinho, kwa sababu ataijenga timu kwa misimu miwili na ataweka moja ya timu kubwa kuwahi kutokea. Atawafanya kuwa wagumu sana kushinda na yeye ni mshindi," **Mchambuzi wa soka wa England, Danny Mills.**





## WASIFU

**JINA KAMILI:** Erling BrautHaaland
**KUZALIWA:** Julai 21, 2000 (miaka 22)
**ALIPOZALIWA:** Leeds, England
**KIMO:** 1.95 m (6 ft 5 in)
**NAFASI:** Straika
**KLABU:** Manchester City
**JEZI:** Namba 9
**TAIFA:** Norway

### VINARA WA ASSISTS

| JINA | TIMU | ASISTI | MECHI |
|---|---|---|---|
| 1. Kevin De Bruyne | Man City | 12 | 25 |
| 2. Bukayo Saka | Arsenal | 9 | 26 |
| 3. Christian Eriksen | Man Utd | 7 | 19 |
| 4. Mohamed Salah | Liverpool | 7 | 26 |
| 5. Andrew Robertson | Liverpool | 6 | 23 |
| 6. Jack Harrison | Leeds Utd | 6 | 24 |
| 7. Bruno Fernandes | Man. Utd | 6 | 24 |
| 8. Martin Ødegaard | Arsenal | 6 | 25 |
| 9. Andreas Pereira | Fulham | 6 | 26 |
| 10. Alex Iwobi | Everton | 6 | 27 |

### VINARA WA UFUNGAJI EPL

1. Erling Haaland (Manchester City) - 28
2. Harry Kane (Tottenham Hotspur) - 18
3. Ivan Toney (Brentford) - 15
4. Marcus Rashford (Man United) - 14
5. Gabriel Martinelli (Arsenal) - 11
6. Aleksandar Mitrovic (Fulham) - 11
7. Mohamed Salah (Liverpool) - 11
8. Miguel Almirón (Newcastle) - 10
9. Rodrigo (Leeds) - 10
10. Bukayo Saka (Arsenal) - 10

### JE, WAJUA?



KATIKA timu zote kwenye historia ya Ligi Kuu England, moja tu imejitokeza kwa kuwa na mbio ndefu zaidi za kutoshindwa nyumbani, nayo ni Chelsea ambayo imecheza mechi 86 bila kupoteza wakiwa Uwanja wao wa Stamford Bridge kati ya Machi 2004 na Oktoba 2008.





# Biteko ampa majukumu matatu Katibu Mkuu mpya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amemkabidhi majukumu matatu ya kuyafanyia kazi Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Kheri Mahimbali, ikiwamo kusimamia malengo ambayo wizara hiyo imepewa na serikali ili yakamilike kwa wakati.

Mahimbali aliteuliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati.

Biteko alitoa maagizo hayo jana jijini hapo, katika kikao cha kumtambulisha Katibu Mkuu huyo kwa watumishi wa idara mbalimbali.

Alisema katika wizara hiyo wapo watu wa aina mbalimbali ambao Katibu Mkuu atakwenda kufanya nao kazi, hivyo anapaswa kuwa makini ili kuhakikisha kazi zinafanyika na kufikia malengo ya serikali kama ambavyo yamepangwa.

"Ndugu katibu mkuu hapa unaowaona wapo watu wa kila aina wapo ambao ukiwapa kazi wao wanaangalia 'dead line' hata kama kazi uliwapa haijakamilika wanakuletea, lakini wapo ambao kazi hawamalizi kwa wakati na wala majibu hawakupi.

"Lakini wapo ambao wao kazi hawafanyi kabisa, lakini wapo wengine ambao wao ukiwapa kazi wanafanya na ukiwarekebisha wanafurahi kurekebishwa, lakini wengine ukiwarekebisha wanakukasilikia,"alisema Biteko.

Naye Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, alisema yapo mambo mengi ambayo wameyafanyia kazi hadi sasa ikiwamo kupunguza idadi ya watu waliokuwa wamekaimu katika nafasi mbalimbali ndani ya wizara hiyo.

# TASAC yatoa ufafanuzi malalamiko vijana kuvunjiwa mikataba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) limekanusha taarifa zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu malalamiko ya vijana zaidi ya 400 waliokuwa wakifanya mafunzo kazi kwenye ukaguzi wa shehena za mizigo bandarini kuvunjiwa mikataba yao bila kufuatwa utaratibu.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Kaimu Mkeyenge, akitoa ufafanuzi huo juzi mkoani hapa kwa waandishi wa habari alisema malalamiko hayo ni pamoja na vijana hao kuvunjiwa mikataba kinyume na utaratibu, huku ikiwa umebaki muda wa mwaka mmoja kuisha.

Alisema malalamiko mengine yaliyotolewa na vijana hao kwenye mitandao ya kijamii ni kufanya kazi bila kukatiwa bima ya afya na TASAC, kutoa rushwa kwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) katika mashauri ya kazi yaliyofunguliwa na vijana hao ili haki isitendeke.

"Hakuna sheria inayomtaka mwajiri yeyote yule kumkatia bima ya afya kijana anayefanya shughuli za mafunzo kazini, suala hilo halipo na hakuna taasisi yeyote inayoweza kufanya hivyo, kwani stahiki zao zimeainishwa kwenye mwongozo wa kitaifa wa mafunzo kazi uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

"Na tuhuma kuhusu TASAC kutoa rushwa kwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ili mashauri ya kazi yaliyofunguliwa na vijana hao haki isitendeke hakuna ukweli wowote,"alisema Mkeyenge.

Mkeyenge alisema vijana ambao mikataba yao ilivunjwa kutokana na mabadiliko ya sheria ni 209 na siyo zaidi ya 400 kama ambavyo inasambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

Alisema vijana hao 209, walivunjiwa mikataba yao baada ya Bunge kufanya marekebisho ya sheria ambayo yaliendelea mpaka kuwasimamia vijana hao na kupeleka mamlaka hayo kwenye sekta binafsi.

"Kati ya vijana 209 waliofutiwa mikataba yao, ni vijana 41 tu ambao hawakuridhika na maamuzi hayo ambapo vijana 32 kati ya vijana 41, shauri lao lilifutwa na CMA kwa kuwa liliwasilishwa nje ya muda, hivyo ni vijana tisa tu ambao shauri lao dhidi ya TASAC lilipokelewa na lipo katika Tume ya Usuluhisi na Uamuzi.

Alisema vijana 168 waliobaki hawakupinga uamuzi wa TASAC wa kuvunja mikataba yao kutokana na mabadiliko ya sheria ambayo yalikuwa ni nje ya uwezo wa shirika.

Aidha, alisema suala hilo lipo kwenye chombo cha maamuzi kisheria, TASAC haipaswi kuzungumzia shauri hilo ila waliona ni busara kulitolea ufafanuzi wa kilichofanyika kwa upande wao na kuacha hatua za maamuzi zinazoendelea kuchukua mkondo wake.

Kadhalika alisema TASAC ni taasisi ya serikali inayosimamiwa na sheria, kanuni na miongozo ya serikali, hivyo mashauri yake kisheria yanasimamiwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ikiwa ni pamoja na shauri hilo, hivyo kwa mantiki hiyo, shirika hilo halijatoa na haliwezi kutoa rushwa yoyote kwa CMA ili kuzuia haki isitendeke kama ilivyoripotiwa katika mitandao ya kijamii.



Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Jeshi la Polisi (DCP), Maria Nzuki (kulia), akipeana mkono na Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Bank of Africa, Nandi Mwiyombella (katikati), baada ya kupokea msaada wa pikipiki tano zenye thamani ya Sh. milioni 13 zilizotolewa na benki hiyo, katika hafla ya kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan iliyofanyika Chamwino Dodoma, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Kamanda wa Polisi Dodoma, Martin Otieno. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# H'shauri yaongeza makusanyo kutoka bil.3.2/- hadi bil.4.6/-

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, imeongeza mapato ya ndani kutoka Sh. bilioni 3.2 mwaka 2021/2022 hadi kufikia Sh. bilioni 4.6 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 43.

Mkurungenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Omary Nkullo, alisema hayo wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari juzi jijini Dodoma, kuelezea majukumu na mafanikio ya halmashauri hiyo kwa miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Dk. Nkullo alisema halmashauri hiyo imefanikiwa kukusanya makusanyo ya ndani zaidi ya Sh. bilioni 3.2 kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 hadi kufikia Sh. bilioni bilioni 4.6 hiyo ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 43.

Alibainisha kuwa hali hiyo inatokana uimarishaji wa vyanzo vya ukusanyaji mapato, kubuni vyanzo vipya na usimamizi madhubuti katika ukusanyaji wa mapato hayo ya halmashauri.

Alitaja mafanikio mengine ya makusanyo hayo kuwa ni uwepo wa mashine za kukusanyia mapato (PoS) zimeongezeka kutoka mashine 77 mwaka 2021 hadi kufikia 97 mwaka 2022/23.

Kadhalika, alisema kwa mwaka 2022/23 hadi Februari 2023, halmashauri hiyo imekusanya mapato ya Sh. bilioni 2.6 toka vyanzo vya ndani sawa na asilimia 58 ya makusanyo.

Pia alisema fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinazotokana na mapato ya ndani zimeongezeka kutoka Sh. milioni 883.5 mwaka 2021/2022 hadi kufikia Sh.milioni 1.1 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 33.4.

Aidha, alisema bajeti ya maendeleo ya sekta ya kilimo kwa kutumia mapato ya ndani imeongezeka kutoka Sh. milioni 97 mwaka 2021 hadi Sh. milioni 337 mwaka 2022/23.

Alisema uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula umeongezeka kutoka tani 102,183 mwaka 2021 hadi tani 214,873 mwaka 2022 na matumizi ya wanyamakazi (maksai) katika kilimo yameongezeka kutoka jozi za maksai 5,032 mwaka 2021 hadi 7,123 mwaka 2022/23.

Aliongeza kuwa matumizi ya matrekta madogo yameongezeka kutoka 45 mwaka 2021 hadi 81 mwaka 2022/23 na matumizi ya matrekta makubwa yameongezeka kutoka 685 mwaka 2021 hadi 752 mwaka 2022/23.

Alisema miradi ya visima virefu, maji ya mtiririko inayofanya kazi imeongezeka toka miradi 52 mwaka 2021 hadi 61 mwaka 2023.

Kuhusu idadi ya watu wanaopata huduma ya majisafi na salama vijijini umbali wa mita 400 alisema imeongezeka kutoka 214,190 mwaka 2021 hadi 355,344 mwaka 2022.

Hata hivyo alisema idadi ya wananchi wanaopata huduma ya majisafi inatarajiwa kuongezeka kufikia watu 378,462 baada ya kukamilika kwa miradi inayoendelea kujengwa katika vijiji sita ambavyo ni Mkoka, Laikala B, Chilanjilizi, Masinyeti, Ijaka, Chamkoroma-Makole inayofadhiliwa na Mfuko wa Maji wa Taifa (NWF) kwa Sh. bilioni 3.8.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliwataka kuendelea kusimamia mapato ili kuongeza huduma kwa wanachi wa halmashauri hiyo.

Alisema kupatikana kwa huduma muhimu kwenye jamii imesaidia kupunguza kero na malalamiko kwa wanachi kwa serikali.





# TacRI yakumbwa uhaba wa miche ya kahawa

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

TAASISI ya Utafiti wa Kahawa nchini (TacRI), kituo cha Mbimba kilichoko Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, kimesema kimeelemewa na mahitaji ya miche ya kahawa kwa wakulima wa zao hilo katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Kimesema sababu hiyo inatokana na uhaba wa fedha pamoja na vitendea kazi kwa ajili ya utafiti na uzalishaji wa miche hiyo, ili kutosheleza mahitaji ya miche kwa wakulima.

Meneja wa TacRI Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dismas Pangalas, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na Nipashe kuhusu maendeleo ya kilimo cha kahawa katika mikoa hiyo.

Alisema wakulima wa kahawa katika mikoa hiyo wanahitaji miche milioni 15 kila mwaka, huku uwezo wa kituo hicho kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kikizalisha miche milioni 3.5 pekee.

Alisema serikali inajitahidi kutenga bajeti kwa ajili ya kituo hicho, lakini malengo hayafikiwi kutokana na fedha hizo kuwa kidogo na kwamba wakati mwingine zinafika kwa kuchelewa hali inayosababisha kituo kushindwa kufikia malengo.

“Shughuli za uzalishaji wa miche ni gharama sana, wakati mwingine tunapata fedha kwa kuchelewa na hivyo tunashindwa kufikia malengo ambayo tumejiwekea kwa mwaka, lakini tatizo la upatikanaji wa vitendea kazi vya kuzalishia miche,” alisema Pangalas.

Alisema uhaba huo wa fedha unasababisha wakose baadhi ya vitendea kazi yakiwamo mashuka meusi ambayo alisema huwa hayapatikani kirahisi.

Alisema pamoja na matatizo hayo bado kituo hicho kimefanya utafiti wa aina 19 za miche bora ya kahawa, ambazo zote zinafaa kwa matumizi ya wakulima katika maeneo yote nchini.

Alisema utafiti wa mbegu hizo umekamilika na zimeshaanza kusambazwa kwa wakulima katika mikoa ya nyanda za juu kusini ambayo ina uhitaji mkubwa.

Alizitaja baadhi ya aina hizo za kahawa kuwa ni pamoja na Compact na N39-3 ambayo mti mmoja unaweza kutoa matunda ya kahawa yenye uzito wa kilo tano, ukilinganisha na kahawa ya awali ambayo wakulima walikuwa wakilima.



Baadhi ya vijana wanaonufaika na programu ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa, chai, matunda na mboga (AGRI-CONNECT) inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) wakiendelea na uvunaji wa chai mwishoni mwa wiki, kwenye moja ya mashamba kwa kutumia mashine za kisasa ambazo zimepelekwa kwa ajili ya kuboresha uvunaji wa zao hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watanzania washauriwa kuacha kutumia bidhaa zisizo na ubora

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATANZANIA wameshauriwa kuacha kutumia bidhaa zisizo na ubora ambazo zinaingizwa nchini kupitia njia za panya, kwamba zinaharibu uchumi wa nchi pamoja na ushindani na bidhaa za ndani.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani (FCC), William Erio, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Haki ya Mtumiaji wa Huduma Duniani ambayo kitaifa yatafanyika jijini humo.

Alisema taasisi yake imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kudhibiti ushindani usiokuwa sawa wa soko hasa kwa kudhibiti uingizwaji wa bidhaa zisizokuwa na ubora.

Alisema tatizo hilo lipo zaidi kwenye mikoa ya mipakani ikiwamo ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini hasa katika mipaka ya Tunduma mkoani Songwe na Kasumulu mkoani Mbeya.

Aliwataka wananchi kutumia bidhaa ambazo zimethibitishwa na taasisi mbalimbali za serikali ikiwamo Shirika la Viwango (TBS) pamoja na kujiridhisha kwa kusoma maelezo ya bidhaa husika.

Alisema ili kudhibiti ushindani wa bidhaa sokoni, wanashirikiana na taasisi mbalimbali za serikali vikiwamo vyombo vya usalama, TBS na Mamlaka ya Mapato (TRA).

Erio alisema maadhimisho hayo ya kitaifa yatatanguliwa na utoaji wa elimu na hamasa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari zikiwamo redio za kijamii.

Alisema maadhimisho hayo yatafanyika Machi 15, mwaka huu, jijini Mbeya na kwamba mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Uwekezaji, Dk. Ashatu Kijaji.

Aliwataka wajasiriamali na wadau mbalimbali wa Mkoa wa Mbeya na mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuhudhuria maadhimisho hayo ili kujua shughuli za taasisi hiyo pamoja na haki wanazostahili.

Baadhi ya wafanyabiashara wa Jiji la Mbeya, waliiomba serikali kuongeza udhibiti wa bidhaa za magendo ili kulinda soko la bidhaa zinazozalishwa ndani.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Safari Mwakabungu, alisema bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia njia za magendo huwa zinauzwa kwa bei ya chini kuliko zile zinazoingizwa kupitia njia halali kwa sababu huwa hazilipiwi ushuru.

Alisema hali hiyo huwa inawafanya wananchi kuzikimbilia kununua na hivyo kufanya ushindani usiokuwa na usawa baina ya bidhaa hizo na zilizo halali.

# CBE yaanza kukabili tatizo ukosefu ajira kwa wahitimu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimeanza kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana nchini kwa kuboresha mitaala yake ili iendane na mahitaji halisi ya soko la ajira pamoja na kuanzisha mitaala mipya itakayowawezesha kujiajiri.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho nchini, Prof. Edda Lwoga, aliyasema hayo juzi alipofanya ziara katika chuo hicho tawi la Mbeya kwa lengo la kujitambulisha kwa wanafunzi na jumuiya ya chuo hicho.

Alisema chuo hicho kimeanzisha atamizi za biashara zinazoanzishwa na wanafunzi kwa lengo la kuzilea biashara hizo ili ziwe endelevu na ziwasaidie vijana hao kujiajiri na kuajiri watu wengine.

Vilevile alisema chuo hicho kimeanzisha uanagenzi kwa ajili ya kuwafundisha vijana wa fani mbalimbali za ufundi zikiwamo za ujenzi, ufundi selemala, ufundi bomba na fani zingine ili ziwasaidie vijana hao kujiajiri.

Kaimu Naibu Mkuu wa CBE Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaaluma, Dk. Nasib Mramba alisema chuo hicho kimekuwa kikifanya utafiti mbalimbali kwa lengo la kulisaidia taifa kupata maendeleo.

Vilevile alisema chuo hicho kimekuwa kikifanya tuafiti kwa ajili ya kubaini uwezo wa wahitimu wake katika kufanya kazi kwenye taasisi zilizowaajiri.

Alisema lengo la utaratibu huo ni kuwafanya wanafunzi kupata uzoefu wa kazi mapema kabla hawajahitimu pamoja na kufanya utafiti ili kujua kama mitaala wanayotumia inakidhi mahitaji.

Mkurugenzi wa CBE Kampasi ya Mbeya, Jeremiah Tumain, alisema wanaendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya chuo hicho baada ya kupata fedha kutoka kwa wadau ambao walichangia wakati wa harambee.

Hivyo, aliwataka wadau kuendelea kuchangia kwa maelezo kuwa bado ujenzi wa kampasi hiyo unaendelea baada ya kutumia majengo ya kupanga kwa muda mrefu.

# Watakiwa kutoa elimu ya kujikinga mvua za masika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WENYEVITI na makatibu wa kamati za maafa wa wilaya za Unguja, wametakiwa kuandaa mipango mikakati ya kuelimisha jamii kuhusu njia bora za kukabiliana na maafa hususani kipindi mvua za masika, ili kuepusha athari.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Salhina Mwita Ameir, alitoa rai hiyo wakati akifungua kikao cha kujadili mwelekeo wa mvua za masika.

Alisema hatua hiyo itasaidia wananchi kujua njia bora za kujiepusha na athari kwa kujikinga na kuchukua hatua stahiki pindi majanga yanapotokea katika maeneo yao.

Ameir alisema kumekuwa na athari nyingi zinazojitokeza katika msimu wa mvua za masika ambazo huathiri watu na mali zao kutokana na mafuriko yanayosababisha uharibifu wa makazi, miundombinu ya barabara, umeme, maji.

Aidha, alieleza kuwa mvua kubwa za masika zinapotokeza kuna maafa yanayojitokeza ambayo hayawezi kuepukika, lakini kuna uwezo wa kupunguza athari iwapo elimu ikitolewa mapema kwa jamii.

Akitoa taarifa ya utabiri wa hali ya hewa, Mwakilishi kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Hassan Khatib Ame, alisema mfumo wa hali ya hewa unaonyesha hivi sasa joto la bahari liko chini.

Aidha, alisema mwelekeo wa mvua za masika kwa Machi hadi Mei kwa visiwa vya Unguja na Pemba vitakuwa na mvua ya wastani hadi juu ya wastani na kuna uwezekano wa mvua hizo kufikia hadi Juni.

Mkuu wa Divisheni ya Mawasiliano na Tahadhari za Mapema, Omar Ali Mohamed alisema mvua za masika zinazotarajia kunyesha zitakuwa kubwa, hivyo ni vyema wananchi kuwa na tahadhari ili kupunguza athari za majanga yanayoweza kujitokeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, Makame Khatib Makame, aliwataka wananchi hasa wale wanaoishi katika maeneo hatarishi kuchukua hatua mbadala ili kujinusuru na maafa.




Mkurugenzi wa Masoko ya Kifedha wa Absa Tanzania, Esther Maruma (wa pili kulia), akizungumza wakati wa kongamano la maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani lililoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wao wanawake jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Ofisa Mkuu Mtendaji wa Institute of Directors in Tanzania (IoDT), Said Kambi, Mtaalamu wa Mawasiliano, Sarah Majengo (kushoto) na Mtaalamu wa Masuala ya Maendeleo ya Fedha, Aida Sykes. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi za muungano zatakiwa kushirikiana utekelezaji miradi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Khadija Khamis Rajab, alisema kunahitajika ushirikiano wa taasisi za muungano katika kufanikisha mipango mbalimbali pamoja na kuwezesha utekelezaji wa miradi yenye tija kwa taifa.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga semina ya siku tano inayohusiana na dhana ya ushirikiano baina ya sekta za serikali na sekta binafsi.

Katibu Mkuu huyo alisema ushirikiano huo wa kisekta kati ya taasisi na taasisi yatasaidia kufanikisha utekelezaji mzuri wa miradi iliopangwa hasa kupitia sekta ya ujenzi na miundombinu tofauti.

Alisema Tanzania imekuwa ikiingia mikataba mbalimbali pamoja na kufanya taratibu za manunuzi, hivyo ni vyema watendaji wake wakajengewa uwezo ili kuwawezesha kuwa na weledi wa kazi za miradi wanayoitekeleza.

Alisema kupitia semina hiyo wizara imeshirikisha washiriki kutoka taasisi mbalimbali kwa Zanzibar na Tanzania Bara kutokana na uhitaji wakati wa kutekeleza miradi, sambamba na kupata mikataba imara isiokuwa na matatizo.

Kwa upande wao washiriki wa mafunzo hayo, Asha Kassim Bakari na Kitainda Maico walisema mafunzo yaliyoyapata yatawasaidia kufanya kazi kwa ufanisi, ikizingatiwa kwa sasa nchi ina mpango maalum wa kutekeleza miradi ya kimkakati.

Pia walisema serikali inaitumia sekta binafsi kama njia mbadala ya kujenga miundombinu kwamba mafunzo hayo yamewawezesha kufanya tathmini katika utekelezaji wa miradi.

## SMZ yaruhusu ufugaji, uzalishaji wa kuku na mazao yake

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema Serikali ya Zanzibar (SMZ), imeruhusu ufugaji na uzalishaji wa kuku ili kupunguza uingizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Aliyasema hayo jana wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa mradi huo eneo la Pangeni Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja.

Shamata aliyataja mazao hayo kuwa ni kuku wa nyama, mayai na kuku wa kienyeji unaotekelezwa na Kampuni ya ZANBREED.

Alisema uwekezaji huo utakapokamilika, wana imani kwamba utaimarisha shughuli za ufugaji wa kuku, hivyo kuweza kulifikia soko la bidhaa za kuku la ndani na nje ya nchi.

Katika ziara hiyo Shamata aliambatana na maofisa mbalimbali katika ziara hiyo akiwamo Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Asha Zahran Mohamed.

Alisema ameridhishwa na utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huo unaohusisha ujenzi wa mabanda sita yenye uwezo wa kuchukua kuku 85,000 kila moja.

"Mradi huu utaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya ufugaji, kwani licha ya kupunguza kwa kiasi kikubwa uagizaji wa nyama na mayai kutoka nje, wafugaji wadogo watapata soko la bidhaa zao lakini pia chakula cha mifugo yao kwa unafuu," alieleza waziri huyo.

Hivyo, alimwomba mkandarasi anayetekeleza mradi huo na uongozi wa Kampuni ya ZANBREED kuukamilisha kwa wakati ili kutoa nafasi ya kuanza kazi na kuwanufaisha wananchi wa Zanzibar katika nyanja mbalimbali ikiwamo ajira.

"Kupitia uwekezaji huu tunaamini wapo wananchi watakopata ajira za muda kama ilivyo hivi sasa na wengine za kudumu utakapokamilika jambo ambalo litaongeza ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na nchi kwa ujumla," alieleza Shamata.

Aidha, Shamata aliwaalika wawekezaji wengine kuja kuwekeza katika sekta zilizomo katika wizara yake ili kufikia lengo la serikali la kuimarisha uwekezaji kama njia mojawapo ya kukuza uchumi na uwezo wa kuwahudumia wananchi.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Asha Zahran Mohamed, aliipongeza kampuni hiyo kwa uamuzi wake wa kuwekeza nchini katika sekta ya ufugaji.

Alisema uwekezaji huo utaongeza thamani ya biashara ya kampuni hiyo kitaifa na kimataifa.

Alieleza kuwa hatua hiyo pia itatanua wigo wa soko la kuku na bidhaa zake lakini huduma za mifugo jamii ya ndege kwa kuongeza upatikanaji wa huduma za matibabu na chakula cha kuku mambo ambayo ni kilio cha wafugaji wengi nchini.

Mhandisi anayesimamia ujenzi wa mradi huo, Ali Salm Ali, alieleza kuwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa mabanda hayo inatarajiwa kukamilika Mei mwaka huu, itafuatiwa na ufungaji wa vifaa kabla ya mradi kuzinduliwa.

Aliongeza kuwa mradi huo unajumuisha uzalishaji wa kuku, mayai, vifaranga na chakula cha kuku, umelenga kupunguza hasara wanayoipata wafugaji kutokana na kupokea vifaranga na bidhaa nyingine za kuku kutoka nje ya Zanzibar.

Mradi huo unatekelezwa na Kampuni ya ZAN BREED inayofanya biashara ya kuingiza nchini bidhaa za kuku, ni miongoni mwa uwekezaji unaofanywa katika maeneo ya yaliyokuwa mashamba ya ng'ombe ya serikali.

# Jackline: Tembo Nickel wametimiza ndoto yangu

## • Mjiolojia aliyependa fani hiyo tangu utotoni

**Na Mwandishi Wetu,** NGARA

WATU waliofanikiwa katika jamii zao, iwe kielimu, kibiashara, kila mmoja ana hadhithi yake ya alipotoka hadi alipo sasa na kilichomvutia au kumshawishi hadi kuamua kutumia njia na mbinu za kufika alipo.

Katika maadhimisho Siku ya Wanawake Duniani, Jackline Bahati, anaeleza alivyoweza kuishi ndoto yake na kufikia alichotamani.

Ni fani ya sayansi inayochunguza maumbile ya dunia na tabia zake za kifizikia na kikemia. Inachungulia pia historia ya dunia na nguvu zinazoendelea kubadilisha maumbile ya dunia.

Binti huyu aliyezaliwa kilomita chache toka ulipo mradi wa uchimbaji wa madini ya Nickel unaoendeshwa na kampuni ya Tembo Nickel wilayani Ngara, anasema moja ya sababu za kusoma fani hiyo ni shughuli alizokuwa akiona zinaendelea kwenye eneo la mradi huo tangu akiwa mdogo.

Kwa sasa ni mmoja wa wana jiolojia wa Tembo Nickel, fani ambayo ni moja ya nguzo muhimu katika shughuli zozote za uchimbaji madini.

Fani hii huchunguza maumbile ya dunia na tabia zake za kifizikia na kikemia. Inachungulia pia historia ya dunia na nguvu zinazoendelea kubadilisha maumbile ya dunia.

Wana jiolojia wanatazama mawe na ardhi wakitafuta maelezo kwa umbo na tabia zake kulingana na kanuni za kisayansi.

Kabla ya uwekezaji wa uchimbaji mali iliyo ardhini, hawa ndiyo wanaoweza kukupa tabia za miamba inayotarajia kuichimba, watakuambia makadirio ya mali iliyo ardhini na pia taarifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na tabia za miamba na athari zake ama faida zake kwa kile unachotaka kukifanya.

Bila taarifa sahihi za kijiolojia, hakuna mradi mkubwa wa uchimbaji unaoweza kufanyika.



Jackline Bahati

Jackline anasema akiwa mwanafunzi wa kidato cha pili, alikuwa hajui kwa undani kinachoendelea katika eneo la mradi, alitamani siku moja aweze kufanya shughuli kama zinazoendelea eneo hilo la karibu na nyumbani kwao ambao kwa wakati huo zilikuwa zaidi ni zile za kijiolojia.

"Elimu ya msingi na sekondari sikusoma huku (Ngara), lakini kwasababu ni kwetu nilikuwa narudi likizo nyumbani, nilivyokuwa kidato cha pili ndio nilianza kupenda shughuli zinazoendelea huku kwenye mradi.

"Nilikuwa sina uelewa sana ya haswa nini kilikuwa kinafanyika huku ingawa nilijua ni shughuli za mgodi, nilitamani nifanye vizuri kwenye masomo yangu na siku moja niwe mmoja wa wataalam wa mambo ya miamba, kwasababu wakati ule tulikuwa tunajua zaidi miamba, kinachofanyika huku ni drilling (uchorongaji wa miamba).

"Nilivyofika kidato cha tatu nikajikuta napenda jiographia, hapa nikaanza kufikiri ni fani gani huko mbele nitakuja kusoma ambayo inaendana na masomo ninayapenda.

"Nilivyofika kidato cha tano, ikabidi nichague mchepuo wa CBG, huko pia nikakutana na rafiki yangu ambaye alikuwa ana dada yake yupo chuo kikuu anasoma jiolojia.

"Huyu aliongeza matamanio yangu ya kuja kuwa mwanajiolojia, tulikuwa tunasoma madaftari yake, nikawa najiambia siku moja ndoto yangu itatimia na naamini nitakuwa mwanajiolojia," anasema Jackline.

Anasema aliongeza juhudi kwenye masomo yake na alihitimu vyema kidato cha sita na kuchaguliwa kusoma jiolojia katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

"Nikiwa mwanafunzi wa mwaka wa pili UDOM, nikaja hapa kwenye mradi kufanya mafunzo kwa vitendo, hapa ndio nikapata picha halisi sasa ya kazi na fani yangu hii.

"Hapa nilikutana na wataalamu hasa waliobobea, kwa kweli walinifundisha mambo mengi na kunifanya ile picha niliyokuwa nayo tangu nikiwa mtoto sasa niione kwa undani wake," anasema Jackline.

Jackline anaamini kila mtu anaweza kuwa kile anachotaka akiwa na nia na kupata watu wa kumwongoza ili kufikia malengo aliyojiwekea.

Anasema watoto wanaozunguka eneo la mradi wa Tembo Nickel hasa wa kike, licha ya changamoto walizonazo, anaamini kila mmoja ataweza kufikia kile anachotaka.

"Ndoto ya mtoto inakuzwa tangu akiwa mdogo, mzazi unatakiwa umnenee mtoto wako mambo mazuri, ambayo yatamfanya naye atamani kufika mbali.

"Sasa familia nyingine unakuta mzazi anataka tu mtoto asiende shule au amalize darasa la saba aolewe ama amsaidie kwenye kazi za kilimo na ufugaji, hiyo ni moja ya changamoto kwetu huku," anasema.

Jackline anaamini watoto wa kike wanaozunguka eneo la mradi, ndoto zao zinaweza kutimia endapo tu watapata watu wa kuwashawishi na kuwaeleza umuhimu wa elimu na kwamba wanaweza kubadili historia za maisha yao na familia zao siku moja.

"Habari za kutia moyo na mifano mizuri inaweza kubadilisha historia za watoto wengi sana huku, mambo ya ndoa za utotoni ama kuzaa ukiwa mtoto yatapungua sana, vizazi vyetu huku vitakuja kuwa hata na vitu vizuri vya kuridhishana.

"Hiyo ni tofauti na sasa ambapo mzazi na mwanafunzi mwenyewe anajua inatakiwa amalize darasa la saba aolewe ama wengine hata hiyo darasa la saba hawafiki.

Hata hivyo, Jackeline anasema, kitendo cha mgodi wa Tembo Nickel kuwa eneo hilo na kuona kwamba kuna wanawake kwenye mgodi huo, tayari ni moja ya jambo linaloweza kubadilisha mtizamo wa watoto wengi wa kike katika mgodi huo.

"Lakini sisi hapa mgodini tumeanzisha jukwaa la wanawake, tunaamini kupitia mambo mbalimbali tunayotarajia kuanza kufanya chini ya mwamvuli wa jukwaa hili, tunaweza kubadilisha historia ya mtoto wa kike anayezunguka eneo hili la mgodi na siku moja akafika mahali ambapo atabadilisha historia yake na familia yake," anasema Jackline.

Akiwa mmoja wa wanawake wa Tembo Nickel, moja ya sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, watapita kwenye shule zinazozunguka eneo la mradi kuzungumza na watoto wa kike masuala mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kuwajengea ujasiri kwamba wanaweza kuwa chochote kwenye maisha yao wakiamua.

"Tutaongea nao mambo mbalimbali ya maisha kwa ujumla, elimu kwa ujumla na mambo ya usafi kwa mtoto wa kike, lengo letu ni kuwajengea ujasiri na kuwaambia kuwa wakiama wanaweza kuwa chochote wanachotamani kwenye maisha yao.

Moja ya maeneo kampuni iliyoanza nayo ni suala la elimu na afya, maeneo ambayo yana nafasi kubwa katika kuinua jamii na hasa mtoto wa kike.

Kupitia mpango wa kurudisha kwa jamii (CSR), kampuni imetekeleza shughuli mbalimbali kwenye sekta ya afya na elimu.

Mbali na kukarabati zahanati kadhaa, kutoa vifaa tiba, Tembo Nickel pia imetoa elimu kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii, ambapo sehemu kubwa ya shughuli zao hushughulikia afya ya mama na mtoto.

Pia kwenye suala la ajira, Tembo Nickel, imekuwa ikitoa nafasi sawa kwa wote, ikiwa ni moja ya njia za kuhakikisha jamii inakuwa na usawa.

Kupitia Siku ya Wanawake Duniani, kampuni ya Tembo Nickel kwa kushirikiana na wadau wengine, ilifanya huduma ya upimaji wa saratani ya matiti kwa wanawake wa Ngara na kuwapa elimu ya kupima ugonjwa huo na mambo mengine.

Jackline ni mfano mmoja kati ya wanawake wengi ambao wameweza kukamilisha ndoto zao bila kurudisha nyuma au kukwazwa kwasababu ya mazingira yao ya ukuaji.

## Ramaphosa apata ushindi kesi ya Phala Phala

**CPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amepata ushindi mdogo katika kesi iliyokuwa ikimkabili baada ya uchunguzi wa mtetezi wa umma anayeamini kuwa hakutumia madaraka yake katika kesi ya Phala Phala.

Inaelezwa kuwa takriban dola 600,000 ambazo awali zilishukiwa, ziligunduliwa kwenye shamba lake moja la mifugo, baada ya wizi mnamo 2020 na kwamba mbinu zilizotumika kurejesha pesa na uhalali wa jumla ni mada ya uchunguzi kadhaa.

Wakati huo huo, uamuzi wa mtetezi wa umma, unatajwa kuwa ni afueni kwa kiongozi huyo ambaye alikuwa karibuni kujiuzulu Desemba 2022, baada ya kuchapishwa kwa ripoti ya uchunguzi isiyofaa.

Inaelezwa kuwa hilo ni wingu moja kubwa chini ya kichwa cha Cyril Ramaphos, na kwamba mtetezi huyo wa umma anaona kwamba rais alitenda ipasavyo katika kuripoti wizi wa shamba lake kwa chifu wa ulinzi wake binafsi, hali ambayo ni sawa na kuripoti kwa polisi, taasisi hiyo inaamini.

Ripoti hiyo inatajwa kuwa ni ushindi mdogo kwa Rais wa Afrika Kusini ambaye anaendelea kutangaza kuwa hana hatia. Bila ya ushindi, rais alijibu kwa kubainisha kwamba Cyril Ramaphosa kamwe hakukiuka kanuni za maadili yake na kwamba katika kesi hiyo, yeye hana hatia.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa kiongozi huyo hajaondolewa kabisa katika kesi hiyo, kwani maswali mengine yanatarajiwa.

Vile vile, inaelezwa kuwa pesa hizo zilitokana na mauzo ya nyati 20 kwa mfanyabiashara wa Sudan na kwamba muamala bado haueleweki na uchunguzi mwingine unaendelea, ukiwamo upelelezi wa makosa ya jinai. **RFI**

# Marekani yahadharisha teknolojia ya China kutumika Afrika

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeendelea kuelezea juu ya wasiwasi wake kuhusu hatari ya nchi za Kiafrika kutumia teknolojia ya China, na ufuatiliaji wa mawasiliano ya simu, ambayo inasema unafanywa na nchi hiyo barani Afrika.


Kundi la wabunge wa Marekani hivi karibuni liliandaa rasimu ya azimio la kukosoa serikali ya Afrika Kusini kwa uhusiano wake wa karibu na Beijing, ikiwa ni pamoja na matumizi yake ya teknolojia ya China na kumtaka Rais Joe Biden kuufanyia tathmini uhusiano wa Marekani na Pretoria.

Hata hivyo, wachambuzi wengine wanasema ni wajibu wa kila serikali kutumia teknolojia kwa uwajibikaji na China sio mdau pekee katika sekta ya teknolojia.

Azimio hilo liliwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi la Marekani wakati Afrika Kusini ikifanya mazoezi ya majini na China na Russia mwezi Februari. Marekani tayari imepiga marufuku matumizi ya vifaa vya kampuni ya teknolojia ya China, Huawei, ikisema ni hatari kwa usalama wa taifa. Pia kuna msukumo kwenye bunge kupiga marufuku programu ya mtandao wa kijamii ya China, TikTok.

Barani Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, inatajwa kuwa chini ya asilimia 30 ya watu wanatumia internet na kwamba serikali nyingi zinakaribisha uwekezaji wa China katika miundombinu ya kidijitali sehemu ya mpango wao uitwao Belt and Road, ambao pia umekuja kujulikana kama Digital Silk Road, yaani barabara ya hariri ya kidijitali.

Kwasababu ya ruzuku ya serikali ya China, nchi hizo zinaichukulia kama njia nafuu ya kuunganishwa zaidi. **VOA**



Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, alipohutubia taifa mjini Cape Town Februari 9, mwaka huu. **PICHA: AP**

# Walimu wagoma Sudan wakidai mishahara

**KARTOUM,** SUDAN

WALIMU katika shule za serikali nchini Sudan wamekuwa kwenye mgomo tangu Novemba 2022, kutokana na mishahara midogo na kutolipwa ujira wao, wakiishutumu serikali kwa kushindwa kuweka kipaumbele kwenye elimu na kwamba wanataka kurejeshwa kwa serikali ya kiraia.

Aidha, wakati wa mgomo na madai hayo yakiendelea nchini humo, waziri wa fedha wa Sudan anasema serikali imekidhi madai ya walimu.

Inaelezwa kuwa shule hazina wanafunzi ambao ni kawaida kuonekana kote nchini humo, ikielezwa kuwa tangu Novemba 2022, walimu wameitisha migomo kadhaa, wakipinga mishahara kwamba katika baadhi ya kesi hawalipwi kwa miezi kadhaa na walimu wanasema ni midogo mno.

Khamis Chatmi ni mkuu wa shule mjini Khartoum, alisema ana wasiwasi kuhusu elimu ya wanafunzi wakati mgomo unaendelea. "Tatizo hili litaharibu vizazi kadhaa na jamii kwa jumla. Tatizo siyo tu linawahusu walimu wa Sudan lakini jamii nzima," alisema Chatmi.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa wanafunzi wa shule binafsi wanaendelea na masomo yao na bado zinafundisha, wakati shule za umma, masomo yamesitishwa, baadhi wa wanafunzi wanaathiriwa wakidai kuwa hiyo ni mbaya kwao kwa kuwa wanataka kuwapo na fursa sawa za kimasomo.

Tangu serikali ya kijeshi inayoongozwa na Abdel Fattah al-Burhan ilipochukua madaraka kwa njia ya mapinduzi Oktoba 2021, maandamano ya kuunga mkono demokrasia yameigubika Khartoum takriban kila siku.

Wafanyakazi wa serikali pia wamekumbwa na kutolipwa mishahara yao.

Wenyeji wa Khartoum na hata baadhi ya maofisa wa serikali waliiambia VOA kuna dhana kwamba serikali haifanyi kazi. Mgomo wa walimu huenda ukawa ni moja ya mambo makubwa.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati wa Walimu, Sudan Gamaria Hussain, ambayo iliandaa migomo, alisema hali hiyo huenda inaweza kusuluhishwa chini ya serikali ya kiraia.

Hussain alisema "kwasababu tulikuwa na serikali ya kiraia ambayo ilijali kuhusu elimu, kinyume na serikali iliyowekwa baada ya mapinduzi. Ni dhahiri baada ya mapinduzi, elimu na nyanja nyingine zimeathiriwa elimu siyo kipaumbele chao hata kidogo kulinga na kile Jibril alichosema katika hotuba yake. Anadhani kwamba elimu na walimu hawana tija."

Jibril Ibrahim ni Waziri wa Fedha wa Sudan, ambaye amekuwa akifanya mashauriano na walimu kwa niaba ya serikali. Akiongea na VOA, alisisitiza kwamba serikali ilishughulikia matatizo ya walimu, ambayo anadai wanadanganya.

"Kwa kweli tumeongeza bajeti kwa elimu kwa kiasi cha asilimia 18 hivi sasa, kwa kiasi jambo zima la madai ya walimu yanahusishwa na siasa. Kwa kweli, madai yao yameshughulikiwa, lakini baadhi wanatumia madai haya kwa ajenda zao za kisiasa," alisema.

Inaelezwa kuwa bado migomo inaendelea, ingawaje mishahara inaonekana kuwa imelipwa kwa walimu mjini Khartoum, hawajalipwa bado katika sehemu nyingine za nchi, kwa mujibu wa walimu.

**VOA**

# RUVU SHOOTING SASA YATAKA KUCHEZA 'PLAY OFF' LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Mbwana Makata, amesema ushindi walioupata Ijumaa iliyopita dhidi ya Mbeya City, umewaongezea ari na kujiamini kwa wachezaji wake, ambapo wataendelea kupambana hata kama wakishindwa kabisa kujiondoa kwenye janga la kushuka daraja basi waangukie japo kwenye mechi za mchujo.

Makata ambaye kwa sasa anapambana ili kuinusuru timu yake, akiipa ushindi wa mabao 2-1 ugenini kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Mbeya City, amesema mechi tano zilizobaki ni nyingi kwao na watatafanya kila njia ili wahakikishe wanatoka eneo hatari.

"Mechi ile ilikuwa ngumu, ila tuliwasoma sana Mbeya City, wanacheza 4-3-3 na sisi tukatumia mfumo huo huo, lakini wao walicheza kwa kushambulia zaidi sisi kwa kushtukiza, ninachoshukuru vijana wangu leo (juzi), wamepata nafasi hizo hizo mbili wamezitumia, nasema haikuwa rahisi kwa sababu jamaa walitaka dakika 20 wawe wamemaliza mechi ndiyo maana tulikaa nyuma na kufunguka kipindi cha pili.

"Yalikuwa ni mabao ya Valentino Mashaka dakika ya 30, Abdulrahaman Mussa dakika ya 81, Sixtus Sabilo akiifungia Mbeya City kwa mkwaju wa penalti akifikisha mabao manane kibindoni.

"Tumepanda kidogo, tukipata ushindi mwingine tutakuwa kule kwenye 'play off', lengo ni kujiondoa kabisa eneo la kushuka daraja, lakini hata kama tukishindwa kabisa basi angalau tuangukie kwenye mechi za mchujo wachezaji wetu wakiendelea kucheza kwa juhudi na maarifa kama hivi hakuna kitakachoshindikana," alisema.

Ruvu Shooting imepanda kutoka kukamata mkia hadi kwenye nafasi ya 15, ikiwa na pointi 20, kabla ya mechi ya jana kati ya Dodoma Jiji dhidi ya Polisi Tanzania.



Kikosi cha Timu ya New City FC, ambayo imepanda daraja msimu huu na sasa kitashiriki Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao wa 2023/24. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# New City yapanda Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya New City imefanikiwa kupanda daraja kutokea Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja na sasa itacheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao wa 2023/2024.

New City imecheza msimu mmoja wa Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja baada ya kutokea Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi msimu uliopita na kufanikiwa moja kwa moja kutinga Ligi Kuu Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Razak Ali Rajab, huku akiwa mwenye furaha alisema hakika malengo makubwa waliyojiwekea yametimia.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na juhudi za wachezaji pamoja na viongozi wa timu hiyo kushirikiana kwa pamoja katika kuhakikisha wanacheza msimu mmoja Daraja la Kwanza na kupanda Ligi Kuu Zanzibar.

Rajab alisema wafuatiliaji wa soka la Zanzibar wanafahamu ugumu mkubwa wa Ligi ya Kanda, na kwamba kwa upande wao walipambana hadi kuhakikisha wanafanikiwa kufikia malengo yao.

"Hakika tunajipongeza na tulistahili kupanda, wachezaji kwa ujumla walijituma na walicheza kwa malengo makubwa na kiu ya kuona wanaipandisha timu daraja imetimia, hakika huu ni ushindi wa wote kuanzia timu mpaka mashabiki zetu," alisema.

New City FC imevuna alama 61 katika michezo 29, iliyocheza ikibakiwa na mchezo mmoja wa kukamilisha ratiba ya Ligi Daraja la Kwanza msimu huu.

Kwa mujibu wa kanuni ya mashindano hayo msimu huu, jumla ya timu nne zitapanda daraja na kucheza Ligi Kuu msimu msimu ujao ambapo timu mbili zitatoka Kanda ya Pemba na idadi kama hiyo Kanda ya Unguja.

Ngome inapewa nafasi kubwa ya kuwa timu ya pili kutoka Kanda ya Unguja kupanda Ligi Kuu msimu huu, hii ni kutokana na kushika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na pointi 57, na imebakisha mchezo mmoja wakati wapinzani wao New King wakiwa na alama 51 huku wakibakisha michezo miwili.

## Kocha Simba Queens amtetea 'Fetty Dansa'

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la Ufundi la Klabu ya Simba Queens, limesema bado lina matumaini na beki wao, Fatma Issa 'Fetty Dansa', licha ya kukaa chumba cha majeruhi kwa muda mrefu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, alisema baadhi ya wadau wa soka wamekuwa wakilalamika kutokana na kiwango cha Fetty Dansa kuonekana kumeshuka tofauti na msimu uliopita.

"Fatma sasa hivi kiwango chake kimeshuka kwa kuwa amekaa nje kwa muda mrefu akiuguza majeraha, mchezaji yeyote akikaa muda mrefu bila kucheza lazima ashuke, ila sina wasiwasi kwa kuwa ni miongoni kati ya wale ninaowategemea katika timu yangu," alisema.

Kuhusu mchezo wao ujao dhidi ya Tiger Queens ya Arusha, utakaopigwa kesho, alisema utakuwa mgumu na wenye ushindani, lakini malengo yake ni kushinda michezo yote ili waweze kutetea ubingwa wao wa Ligi Kuu ya Wanawake.

## Wazo Jipya Cup yarindima Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

LIGI ya mpira wa miguu ya Wazo Jipya Bakery Super Cup iliyoshirikisha timu 16 wilayani Muheza, Tanga imeanza kutimua vumbi rasmi.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, Desderia Haule, akimwakilisha Mkuu wa wilaya hiyo, Juma Irando, alifungua ligi hiyo juzi jioni katika Uwanja wa Jitegemee wilayani hapo ambapo timu ya Bich Boy ya Muheza iliibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Saruji FC ya jijini Tanga.

Akizungumza katika ufunguzi huo, Katibu Tawala huyo alisema ligi hiyo ina lengo la kukuza vipaji kwa vijana wa Muheza lakini kuwawezesha kujichanganya ili kuwaepusha na mambo mengi maovu kama ukabaji na utumiaji dawa za kulevya.

Aliwataka vijana kucheza kwa bidii, nidhamu na kuonesha unyenyekevu katika ligi hiyo ili wakuze vipaji vyao vya mpira na kusonga mbele kwa kuwa mpira kwa sasa ni ajira.

Kwa upande wa Meneja wa Wazo Jipya Bakery wilayani Muheza, John Simon, alisema wameidhamini ligi hiyo kwa kushirikiana na Zahanati ya Daty ambapo inashirikisha jumla ya timu 16, mbili kutoka Tanga mjini na 12 Muheza.

Simon alitaja zawadi ambazo zitatolewa siku ya fainali kuwa mshindi wa kwanza atapata Sh. 800,000 wa pili Sh. 400,000 na mshindi wa tatu ataondoka na Sh. 200,000.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PICKFORD ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili golikipa wa England, Jordan Pickford, kipindi cha majira ya joto, ingawa kipa huyo mwenye umri wa miaka 29, ndio kwanza amesaini mkataba wa muda mrefu na Everton. (***Sun***)

### PSG YAMWANIA HAALAND

PARIS St-Germain inaweza kumtaka kumsajili, Erling Haaland kutoka Manchester City ili nyota huyo wa Norway mwenye umri wa miaka 22, asaidiane na Kylian Mbappe, 24. (***RMC Sport, via Sport***)

### JONG KIPAUMBELE CHELSEA

CHELSEA imemfanya kiungo wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 25, kama kipaumbele chao cha usajili wa kipindi cha majira ya joto. (***Football Insider)***

### FELIX ANOGEWA

FOWADI wa Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23, ana furaha na Chelsea ambako anacheza kwa mkopo na klabu hiyo itazungumza na Atletico Madrid kuhusu mkataba wa kudumu kipindi cha majira ya joto. (***Relevo***)

### GERRARD KUINOA TRABZONSOR

KOCHA wa zamani wa Aston Villa, Steven Gerrard, amepaa kwenda Istanbul nchini Uturuki kufanya mazungumzo na Klabu ya Trabzonspor ili kuwa kocha mpya. (***Karar***)

### KANE GHALI ZAIDI

MANCHESTER United inajiandaa kutoa ofa ya kumfanya Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, kuwa mchezaji ghali zaidi wa muda wote kwenye historia ya soka la Uingereza kipindi cha majira ya joto. (***Mirror***)

### NDIAYE AWINDWA EVERTON

EVERTON inawania kumsajili fowadi wa Sheffield United na Senegal, Iliman Ndiaye, mwenye umri wa miaka 23. (***Sun***)

### TORRES ATAJWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inawania kumsajili nyota wa Villarreal, Pau Torres, mwenye umri wa miaka 26, mwaka mmoja baada ya Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, kujaribu kushawishi ajiunge naye, 26. (***Mirror***)

### MSHAHARA KUMZUIA MAGUIRE

MANCHESTER United inahofia haitakuwa na uwezo wa kumuuza mlinzi wa England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 30, kipindi cha majira ya joto kutokana na mshahara wake, ambapo ni zaidi ya pauni 200,000 kwa wiki. (***Football Insider***)

### SILVA BASI TENA BARCA

BARCELONA inaweza kuachana na mpango wa kumsajili Bernardo Silva kwa sababu Manchester City itataka pauni milioni 70 ili kumwachia kiungo huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 28. (***Mundo Deportivo***)

### ALVAREZ AKIFUNGA CITY

MANCHESTER City inakaribia kufikia makubaliano ya kuongeza mkataba mpya na straika wa Argentina, Julian Alvarez, mwenye umri wa miaka 23, ambao sasa utamfanya kukaa na klabu hiyo hadi mwaka 2028 na mshahara mnono zaidi. (***TyC Sports***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# VINICIUS JR ALIA WAAMUZI WA LALIGA KUTOMLINDA

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Vinicius Junior, amewakosoa waamuzi wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa kushindwa kutoa kadi kwa wapinzani wanaomchezea vibaya mara kwa mara.

**Vinicius alifunga wakati Madrid ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Espanyol Jumamosi, hilo likiwa ni bao lake la 19 katika mechi 39 alizocheza msimu huu.**

Kwa mara nyingine alilengwa na wachezaji wa timu pinzani, huku akifikisha faulo 138 alizofanyiwa katika mashindano yote msimu huu, zikiwa 34 zaidi ya mchezaji mwingine yeyote katika ligi tano bora za Ulaya.

Lakini Vinicius mwenyewe alioneshwa kadi ya 12 ya njano msimu huu dhidi ya Espanyol - ni Sofyan Amrabat (13) na Alex Baena (14) pekee ndio wenye kadi nyingi zaidi yake.

"Waamuzi hawaangalii faulo ninazofanyiwa na hawatoi kadi za njano," alisema akiiambia ESPN.

"Wachezaji wanaweza kunifanyia madhambi mara 15 na mchezo ukiwa katika dakika ya 88, mwamuzi anatoa njano. "Wachezaji wanapaswa kufikiria njia ya kunizuia na kwa kufanya faulo inakuwa rahisi sana kwao.

"Siwahukumu wachezaji, lakini nawahukumu waamuzi, kwa sababu wanapaswa kutumia kanuni kwa usahihi."

Vinicius aliongeza: "Siombi mtu yeyote anilinde. Hakuna mtu ambaye amenilinda katika maisha yangu, isipokuwa wachezaji wenzangu, wazazi wangu na watu wanaonipenda.

"Ninachopaswa kufanya ni kujaribu kuweka mambo wazi. Ninafanya makosa wakati mwingine; nina umri wa miaka 22 tu.

"Nitafanya makosa mengi. Lakini nataka kufanya makosa machache na kuendelea kujifunza."

> ●●● Wachezaji wanapaswa kufikiria njia ya kunizuia na kwa kufanya faulo inakuwa rahisi kwao, lakini...

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 508

MECHI KALI
IHEFU FC
VERSUS
AZAM
1 | 4.65
X | 3.41
2 | 1.69

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# KLOPP: BOURNEMOUTH IMESTAHILI USHINDI

**LONDON,** England

KOCHA Jurgen Klopp, alikubali kwamba, Bournemouth ilistahili ushindi wao wa bao 1-0 dhidi ya Liverpool baada ya 'Wekundu' hao kukosa nafasi ya kuingia kwenye nne bora ya Ligi Kuu England.

Juhudi za kipindi cha kwanza za Philip Billing zilitosha kukishusha kikosi hicho cha Merseyside kwenye Uwanja wa Vitality, kwa pointi tatu na kuwaondoa kutoka eneo la kushushwa daraja.

Mohamed Salah, aliyetoka kufunga mabao mawili katika mchezo wa Jumapili iliyopita wa 7-0 dhidi ya Manchester United na kumfanya mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri kuwa mfungaji bora wa muda wote wa Liverpool kwenye Ligi Kuu, alikosa penalti kipindi cha pili.

Klopp anaamini hiyo ingeweza kuwa hatua ya mabadiliko katika mchezo huo, ingawa alihisi Bournemouth, ambao waliwapa viongozi Arsenal hofu mara ya mwisho, walikuwa wamechelewa kupata ushindi kwa muda mrefu.

"Penalti ya mwisho tuliyopata tungefunga mchezo ungeweza kugeuka," alisema Klopp akiiambia BT Sport.

"Haifanyi matokeo kuwa bora, lakini inaweza kubadilisha matokeo angalau, anafunga mabao, anafunga mabao mengi, lakini alikosa penalti, hayo ni maisha.

"Ilikuwa wazi tangu sekunde ya kwanza tunakuja hapa, Bournemouth wanapigania kubaki kwenye ligi, klabu ya ajabu, jiji la ajabu, wanataka kubaki ndani na wanafanya vizuri sana.

"Matokeo hayakuwa yakienda sawa katika miezi michache iliyopita, lakini maonyesho yanaonekana tofauti, na kwa hivyo walistahili alama tatu leo (juzi)."

# Haaland: Hakuna mechi rahisi Ligi Kuu

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Erling Haaland, amekubali kwamba, hakuna mechi rahisi katika Ligi Kuu England baada ya bao lake la 28 kwenye ligi hiyo msimu huu kuwezesha ushindi wa 1-0 dhidi ya Crystal Palace, Jumamosi.

Penalti ya Haaland katika dakika ya 78, iliipatia City ushindi muhimu katika mbio za kuwania taji hilo pale kwenye dimba la Selhurst Park baada ya Palace kuwabana mabingwa hao watetezi kila idara.

Wakati Haaland alifarijika kupata ushindi huo, alitolea mfano ugumu wa ligi hiyo baada ya Liverpool kuchezea kichapo cha bao 1-0 mapema siku hiyo kutoka kwa Bournemouth.

"Mwisho cha muhimu ni pointi tatu," alisema akiiambia Sky Sports. "Siyo rahisi. Kila mchezo mmoja si rahisi. Uliona Bournemouth wakiifunga Liverpool. Kila mechi moja ni pambano na umeliona hilo kwa City, na tulishinda na nina furaha sana."



Hakuna mchezaji aliyefunga penalti nyingi za Ligi Kuu msimu huu kuliko Haaland (tano sawa na Ivan Toney wa Brentford), wakati Yaya Toure pekee ndiye aliyefunga penalti nyingi zaidi kwa msimu mmoja akiwa na City (sita msimu wa 2013-14).

Vijana wa Pep Guardiola walilazimika kutoka nyuma kwa mabao 2-0 na kuishinda Palace 4-2 katika mechi ya marudiano Agosti mwaka jana ambayo kwa mujibu wa Haaland, ndiyo sababu yeye na wachezaji wenzake hawakuwa na hofu wakati mechi yao ya Jumamosi ilipokuwa haina bao.

"Sikuwa na wasiwasi, nilijaribu kufanya kama ninavyofanya kila mchezo na hiyo ilikuwa kuzingatia mchezo wangu," alisema.

"Mechi ya mwisho dhidi ya Palace tulikuwa nyuma kwa 2-0 na safari hii tulikuwa 0-0, kwa hiyo si mbaya, ilibidi tuendelee. Kama nilivyosema, si rahisi, lakini ninajivunia ushindi."

Haaland alikosa nafasi katika dakika ya 28 alipounganisha krosi ya Nathan Ake na kupaisha juu ya goli.

"Bila shaka sipendi kukosa nafasi," alisema. "Nilikuwa na moja katika kipindi cha kwanza ambacho nilipaswa kufunga, ni jambo dogo lilifanya mpira kudunda juu kidogo, lakini ningefanyaje?

"Lazima niendelee na kujaribu kupata nafasi inayofuata, na nilipata nafasi yangu na nikafunga na tukashinda, kwa hiyo nina furaha."

City wamo pointi mbili pekee nyuma ya Arsenal kileleni mwa jedwali, huku 'Washikabunduki' hao jana Jumapili walisafiri kucheza na Fulham.

## HABARI MICHEZO


,027,160

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/03/23 | 23:00 | Porto vs Inter | 2.60 | 3.30 | 2.49 |
| 02. 15/03/23 | 02:05 | Tlaxcala FC vs Venados FC | 2.58 | 3.15 | 2.53 |
| 03. 15/03/23 | 04:10 | Independiente Santa Fe vs America De Cali | 2.27 | 3.06 | 3.01 |
| 04. 15/03/23 | 06:05 | Correcaminos Uat vs Tepatitlan FC | 2.24 | 3.11 | 3.01 |
| 05. 15/03/23 | 19:30 | NK Celje vs Olimpija Ljubljana | 2.62 | 3.23 | 2.39 |
| 06. 15/03/23 | 22:30 | Southampton vs Brentford | 2.85 | 3.15 | 2.38 |
| 07. 15/03/23 | 23:00 | Real Madrid vs Liverpool | 2.33 | 3.46 | 2.68 |
| 08. 16/03/23 | 20:45 | Fenerbahce vs Sevilla FC | 2.23 | 3.37 | 3.16 |
| 09. 16/03/23 | 20:45 | Djurgardens IF vs Lech Poznan | 2.46 | 3.27 | 2.72 |
| 10. 16/03/23 | 20:45 | Slovan Bratislava vs FC Basel | 2.47 | 3.23 | 2.73 |
| 11. 16/03/23 | 23:00 | AZ Alkmaar vs Lazio | 2.83 | 3.28 | 2.37 |
| 12. 16/03/23 | 23:00 | Union Saint Gilloise vs Union Berlin | 2.77 | 3.32 | 2.39 |
| 13. 16/03/23 | 23:00 | Real Sociedad vs Roma | 2.19 | 3.27 | 3.32 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 13/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1196 | Dire Dawa Kenema FC vs Legetafo Legedadi | 1.63 | 3.30 | 4.50 |
| 16:00 | 1420 | Al Jabalain vs Al Qadisiyah | 2.56 | 2.83 | 2.73 |
| 16:00 | 2429 | Ihefu FC vs Azam | 4.03 | 2.95 | 1.46 |
| 16:15 | 2173 | Panserraikos vs Niki Volou | 1.68 | 3.26 | 5.07 |
| 17:00 | 1655 | ATK Mohun Bagan vs Hyderabad FC | 2.21 | 3.23 | 2.87 |
| 17:00 | 2876 | Al-Shamal-Umm vs Salal SC | 2.62 | 3.28 | 2.36 |
| 17:00 | 4854 | Sheriff Tiraspol vs FC Balti | 1.24 | 4.50 | 9.40 |
| 17:30 | 2756 | Kustosija vs NK Jarun Zagreb | 2.41 | 3.19 | 2.62 |
| 18:00 | 1910 | Sigma Olomouc B vs SK Prostejov | 2.13 | 3.23 | 3.02 |
| 18:25 | 2390 | Alshoulla vs Najran SC | 2.39 | 2.82 | 2.97 |
| 18:30 | 1098 | Chindia Targoviste vs Voluntari | 2.42 | 2.93 | 2.98 |
| 18:30 | 2063 | Kolubara vs Backa Topola | 3.69 | 3.18 | 1.91 |
| 18:30 | 2973 | Al Hala Muharraq vs Al Ahli Manama | 2.23 | 2.95 | 3.21 |
| 18:30 | 5850 | Riffa Club vs Al Hidd Club | 1.32 | 4.57 | 8.10 |
| 18:55 | 1629 | AL Arabi (SA) vs Al Orubah | 1.98 | 2.90 | 3.45 |
| 19:00 | 3840 | AEL Limassol vs Olympiakos Nicosia | 1.85 | 3.33 | 4.18 |
| 19:00 | 4693 | Fasil Kenema vs Welayta Dicha FC | 1.81 | 2.90 | 4.10 |
| 19:00 | 5749 | Racing Club Dabidjan vs ASEC Mimosas | 7.65 | 3.88 | 1.41 |
| 20:00 | 1157 | El Fahem vs Hapoel Ramat Gan | 1.88 | 3.22 | 4.22 |
| 20:00 | 1799 | Istanbulspor vs Sivasspor | 3.10 | 3.26 | 2.20 |
| 20:00 | 2060 | AEK Larnaca vs Apollon Limassol | 1.89 | 3.38 | 3.91 |
| 20:00 | 2860 | Hapoel Afula vs Hapoel Petah Tikva | 2.51 | 3.16 | 2.74 |
| 20:00 | 3065 | Eyupspor vs Altay | 1.37 | 4.32 | 6.79 |
| 20:00 | 4826 | Arka Gdynia vs Gornik Leczna | 1.60 | 3.74 | 4.61 |
| 20:00 | 5547 | Maccabi Petach Tikva vs Hapoel Acre | 1.73 | 3.69 | 4.33 |
| 20:00 | 5647 | Samsunspor vs Bandirmaspor | 1.70 | 3.70 | 3.95 |
| 21:00 | 3239 | Wisla Plock vs Widzew Lodz | 2.73 | 3.09 | 2.39 |
| 21:00 | 4631 | MTK Budapest vs Diosgyori Vtk | 2.26 | 3.19 | 2.83 |
| 21:00 | 5125 | Hammarby vs AIK Football | 1.96 | 3.37 | 3.42 |
| 21:00 | 5239 | Randers vs Aarhus | 2.54 | 3.04 | 2.84 |
| 21:30 | 1581 | Hapoel Tel Aviv vs Maccabi Haifa | 6.79 | 4.32 | 1.37 |
| 21:30 | 5677 | CFR Cluj vs Universitatea Cluj | 1.63 | 3.55 | 5.12 |
| 22:00 | 1328 | De Graafschap vs PEC Zwolle | 3.24 | 3.55 | 1.98 |
| 22:00 | 1571 | Almere City vs VVV Venlo | 1.84 | 3.59 | 3.65 |
| 22:00 | 1592 | Roda Kerkrade vs Jong AZ Alkmaar | 1.79 | 3.59 | 3.90 |
| 22:00 | 1703 | Jong Utrecht vs Jong PSV | 2.39 | 3.33 | 2.65 |
| 22:00 | 2380 | FC Eindhoven vs ADO Den Haag | 2.10 | 3.33 | 3.13 |
| 22:00 | 5033 | NAC Breda vs Jong Ajax | 1.89 | 3.69 | 3.38 |
| 22:30 | 1387 | The New Saints vs Bala Town | 1.22 | 5.57 | 10.11 |
| 22:30 | 4948 | Crotone vs Catanzaro | 2.93 | 3.09 | 2.47 |
| 22:45 | 1751 | Falkirk FC vs Ayr United | 2.35 | 3.37 | 2.65 |
| 22:45 | 4003 | Bradford PA vs Alfreton | 4.03 | 3.41 | 1.79 |
| 22:45 | 4006 | AC Milan vs Salernitana | 1.24 | 5.41 | 10.01 |
| 22:45 | 4123 | Metz vs Le Havre | 2.24 | 2.90 | 3.35 |
| 22:45 | 4819 | Crusaders Belfast vs Cliftonville Belfast | 1.94 | 3.44 | 3.29 |
| 23:00 | 1646 | FC Versailles 78 vs Bastia Borgo | 1.46 | 3.95 | 6.74 |
| 23:00 | 2014 | Racing Santander vs Huesca | 2.34 | 2.86 | 3.21 |
| 23:00 | 3314 | San Telmo vs San Martin Tucuman | 3.76 | 3.02 | 1.99 |
| 23:00 | 4369 | Girona vs Atletico Madrid | 3.40 | 3.25 | 2.05 |
| 23:15 | 3275 | Famalicao vs Casa Pia Atletico | 2.08 | 3.17 | 3.47 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SIMBA YAMWAHIDI RAIS SAMIA MAKUBWA ZAIDI KWA HOROYA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro juzi, uongozi wa klabu hiyo umesema ni jambo zuri kuwa na rais wa nchi anayependa michezo kiasi cha kuongeza motisha katika ufungaji magoli muhimu ya kuzivusha timu za nchi yake kwenye michuano ya kimataifa.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ameahidi shilingi milioni tano kwa kila bao linalofungwa na wawakilishi wa nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, Simba na Yanga, ahadi ambayo amekuwa akiitekeleza ziwe zinachezа nyumbani ama ugenini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Msemaji wa Simba, Ahmed Ally, alisema si tu Rais Samia anatamani timu za Tanzania zifanye vizuri kimataifa, bali pia anashiriki kikamilifu katika mbinu ya utafutaji wa mabao muhimu ya kuzisaidia timu za nchi yake.

Alisema hali hii inaongeza chachu ya wachezaji, mashabiki, wanachama na viongozi wote kuona wana deni kubwa kwa rais wao, hivyo kuongeza bidii kubwa katika ushindi wa mechi zao. "Si tu Rais Samia anataka twende mbele, bali pia anaingia kwenye watafutaji wa magoli, kwa maana kununua goli katika mechi ngumu kama hizi, anamaanisha anataka wachezaji wacheze jihadi ili kuyapata kwa lengo moja tu timu ishinde na kupata pointi muhimu.

"Mambo kama haya kufanywa na mtu mkubwa kama rais wa nchi yanatia moyo, ukizingatia anayefanya haya si mtu wa kawaida isipokuwa raia namba moja kwenye taifa letu, hivyo sisi Simba tunamwahidi makubwa mama yetu kwenye mechi yetu dhidi ya Horoya Jumamosi ijayo kwa lengo moja la kufuzu robo fainali," alisema Ally.

Ahadi hiyo ya Rais Samia, aliitoa kuelekea mechi za raundi ya pili baada ya Simba inayoiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na Yanga Kombe la Shirikisho, zote kuanza kwa kupoteza ugenini mechi zao za hatua ya makundi.

Simba ilianza kwa kupoteza kwa bao 1-0 ugenini nchini Guinea dhidi ya Horoya AC, wakati Yanga nayo ikiwa nchini Tunisia, ilikubali kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya US Monastir.

Hata hivyo, michezo ya raundi ya pili nyumbani hali ilizidi kuwa mbaya kwa Simba baada ya kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya Raja Casablanca wakati Yanga ikibeba milioni 13 za Mama kutokana na ushindi wao wa 3-1 dhidi ya TP Mazembe.

Michezo iliyofuata Simba iliambulia milioni tano kutokana na ushindi wa bao 1-0 ugenini Uganda dhidi ya Vipers huku ikitoka tena na kitita kama hicho iliporudiana na miamba hiyo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam baada ya kupata ushindi kama huo.

Kwa Yanga ilikomba tena milioni tano kutokana na kupata sare ya bao 1-1 dhidi ya Real Bamako ugenini nchini Mali kabla ya kuondoka na milioni 10 ilipoichapa mabao 2-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi ya marudiano.

Kwa ujumla hadi sasa Rais Samia ameshatoa Sh. milioni 40, Yanga ikivuna milioni 30 na Simba milioni 10, kutokana na jumla ya mabao nane timu hizo kwa pamoja ziliyofunga.

**BEN POL...**



Mwanamuziki Bernard Paul maarufu Ben Pol (mwenye suti nyeusi), akiimba nyimbo ya asili ya kabila la Wagogo ambalo ndio kabila lake, sambamba na kikundi cha Mchoya cha Kijiji cha Nazli wilayani Chamwino kwenye tamasha la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, lililofanyika Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma mwisho mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kocha atoa siri hat-trick ya Baleke

INATOKA UK 24

awezekana kabisa huko mbele yakawasaidia. Simba imefunga mabao 58 mpaka sasa na inaongoza kwa kupachika mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

"Sisi kama makocha tunafurahi sana timu yetu inapofunga mabao mengi kwa sababu mwisho wa siku mbele ya safari yatatusaidia pale ambapo huenda pointi zinaweza kulingana," alisema.

Naye mfungaji wa mabao yote 'hat-trick', Baleke, baada ya kukabidhiwa mpira wake na mwamuzi Jonesia Rukyaa alisema: "Nina furaha ambayo siwezi kuelezea kwa sababu hii ni mara ya kwanza kufunga hat-trick nikiwa Tanzania. Huu ni uthibitisho kuwa tutafanya vema kwenye mechi zetu zinazokuja za kimataifa na Ligi Kuu," alisema mchezaji huyo ambaye anafikisha bao la tano kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwa amesajiliwa kipindi cha dirisha dogo akitokea Klabu ya Nejmeh SC ya Lebanon aliyokuwa akicheza kwa mkopo kutoka TP Mazembe.

Naye Saido Ntibanzonkiza alisema ushindi huo utawapa nguvu wao kama wachezaji na mashabiki wa Simba kuelekea kwenye mechi ya Jumamosi dhidi ya Horoya.

Alisema kuwa kama wasingeshinda, wangewahuzunisha mashabiki wao na ndiyo maana waliingia kwa nguvu kubwa kusaka mabao ya mapema na kweli wakayapata.

"Tumepata ushindi na tumecheza mpira mkubwa sana, mwalimu alituambia tuingie kucheza kwa kasi ili tupate mabao ya mapema na kweli ikawa hivyo, baada ya hapo tulitulia, siyo kwa sababu hatukutaka kufunga, ila tulipunguza kasi kwa sababu tayari tulikuwa na kitu mkononi, tukaanza kutembeza boli," alisema kiungo huyo.

Nahodha wa kikosi cha Mtibwa Sugar, Issa Rashid 'Baba Ubaya' alisema kipindi cha kwanza walikosa umakini ndiyo maana wapinzani wao walipata mabao ya haraka.

Matokeo hayo yanaifanya Simba kufikisha pointi 57, ikiendelea kuwa kwenye nafasi ya pili, huku Mtibwa ibaki nafasi ya tisa na pointi zake 29.

# Michezo


Nipashe

Jumatatu Machi 13, 2023




Haaland: Hakuna mechi rahisi Ligi Kuu UKURASA 22

HAT-TRICK...




Mwamuzi wa kati, Jonesia Rukyaa (kushoto), akimkabidhi zawadi ya mpira mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke, baada ya kufunga mabao matatu (hat-trick), kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mtibwa Sugar iliyopigwa Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro juzi. **MPIGAPICHA WETU**

## Kocha aanika siri hat-trick ya Baleke

**Na Adam Fungawango**

MABAO matatu 'hat-trick' aliyofunga straika Jean Baleke wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro, yametoka katika uwanja wa mazoezi, kwa mujibu wa Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda.

Akizungumza na mwandishi wetu, Mgunda alimsifu Baleke kuwa ni mshambuliaji aliyekamilika na kwamba ataendelea kufanya vizuri kwa kushirikiana na wenzake kikosini.

"Tunashukuru tumepata ushindi, mchezaji wetu Jean Baleke amefunga mabao yote, yule ni mfungaji aliyekamilika, vile vitu ambavyo amevifanya kwanza tumejifunza kwenye viwanja vya mazoezi, ndivyo ambavyo tuliwakumbusha wachezaji wavifanye leo, na yeye ameweka ya kwake binafsi ndiyo unaona kilichotokea.

"Ilikuwa mechi muhimu kwa sababu tulikuwa tunataka pointi tatu ili kuufukuzia ubingwa, wapo wanaoona kama hatuwezi au ni ngumu, siku zote haiwi mwisho hadi ifike mwisho, bado tupo kwenye njia za ubingwa, tulihitaji ushindi ili tuwe bado kwenye mbio hizo, tumepata tunajipanga na mchezo mwingine kwa sababu haya ni mashindano ya kutafuta bingwa wa nchi," alisema Mgunda.

Kuhusu Moses Phiri kushindwa kufunga mabao kwa siku za karibuni, Mgunda alisema kuwa mchezaji huyo bado alikuwa majeruhi na bado hajarudi kwenye asilimia zake 100 za utimamu na ubora, lakini kuna mapungufu ambayo wameyaona na wao kama makocha ndiyo kazi yao watayarekebisha.

Mgunda pia ameonyesha kufurahishwa na timu yake kuendelea kufunga mabao mengi ambayo in-

INAENDELEA UK 23

# MAYELE AANZA KUIGUSA SIMBA

**Na Saada Akida**

## ●●● Ni wakati wakisaka pointi 18 za kufunga msimu wa Ligi Kuu, lakini akata tamaa kuishika rekodi ya...

WAKATI miamba ya soka nchini, Simba na Yanga kila moja ikibakiza mechi moja kabla ya kukutana Aprili 16, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, mshambuliaji wa vinara hao wa Ligi Kuu Bara, Fiston Mayele, ametangaza hali ya hatari ya kucheka na nyavu.

Kwa mujibu wa ratiba ya Ligi hiyo, Yanga itaikaribisha Kagera Sugar Aprili 7, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kesho yake Simba itakuwa ugenini mkoani Mbeya kuvaana na Ihefu FC na baada ya michezo hiyo, mechi itakayofuata itakuwa Aprili 16, mwaka huu, kwa miamba hiyo kuvaana.

Hata hivyo, kuelekea michezo sita ya ligi hiyo iliyobaki kwa miamba hiyo kabla ya ligi kufikia ukingoni, Mayele amewatangazia wapinzani wao kuwa malengo yao ni kutaka kukusanya pointi 18 katika mechi hizo zilizosalia.

Kabla ya mchezo wa jana dhidi ya Geita Gold FC uliopigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, Yanga watakuwa na michezo sita iliyosalia ya ligi hiyo ikiwamo dhidi ya Kagera Sugar utakaopigwa Chamazi na Simba Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mechi zingine dhidi ya Singida Big Stars utakaopigwa katika Uwanja wa Liti mjini Singida, Dodoma Jiji FC utakaopigwa Dimba la Azam Complex na michezo miwili itakayopigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Mbeya City na Tanzania Prisons, ambayo yote Mayele amepania kuipa timu yake alama tatu kila mmoja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mayele alisema mikakati yao ni kushinda mechi zote zilizopo mbele yao ili kuendelea na rekodi yao ya kutopoteza mechi tangu Novemba 29, mwaka jana walipokubali kipigo cha mabao 2-1 ugenini dhidi ya Ihefu FC. Alisema wapinzani wao watakaokutana nao wajiandae vizuri kwa sababu mikakati yao ni kuendeleza rekodi ya kutopoteza pointi yoyote katika michezo sita iliyosalia ya ligi hiyo.

"Ligi imekuwa ya ushindani na sasa tunaelekea ukingoni mwa msimu, wapinzani wetu wajiandae vizuri kwani dhamira yetu ni kushinda mechi zote sita na kuvuna pointi 18, suala la kuwania tuzo ya ufungaji bora bado lipo palepale.

"Kwa sasa kipaumbele changu ni kuona Yanga inapata matokeo mazuri katika michezo sita iliyosalia kwa kukusanya pointi zote 18 ili kutetea taji la ubingwa baada ya hapo ndio mambo ya ufungaji bora yanafuata," alisema Mayele.

Alisema kwake binafsi muhimu sana ni malengo ya timu kwa sababu wanahitaji kutwaa ubingwa kwa mara nyingine msimu huu.

Mayele alisema mshambuliaji yeyote lazima awe na malengo binafsi na kwamba kwa sasa michezo iliyosalia hawezi kufunga mabao mengine 11 ili kufikia rekodi ya nyota wa zamani wa Yanga, Mohamed Hussein 'Mmachinga' aliyoiwekwa 1997 ya kufunga mabao 26 katika mechi 24 tu za ligi hiyo.

Hadi sasa Mayele ameshacheka na nyavu mara 15, hivyo kwa mechi zilizosalia inaonekana pia itakuwa vigumu kufikia hata rekodi ya Abdalah Juma (Mtibwa) ya mabao 25 mwaka 2005, Meddie Kagere (Simba) mabao 23 msimu wa 2018/19, Amissi Tabwe (Yanga) mabao 21 msimu wa 2015/16 na Emanuel Okwi (Simba) mabao 20 msimu wa 2017/18.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042